**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO BAJETI KUU YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**DKT. JUMA MALIK AKIL (MBM)**

**JUNI, 2026**



***Ninawashukuru wananchi wote kwa kuendeleza amani, utulivu na mshikamano. Niwaombe tuendelee kulinda tunu hizi muhimu, kwani maendeleo ya nchi yetu yanategemea zaidi umoja wetu na utulivu wa kisiasa.***

***Dkt. Hussein Ali Mwinyi***

***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.***

## YALIYOMO


A. UTANGULIZI ........................................................................ 1

B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI JULAI 2025 – MACHI, 2026 ............................................ 6

B.1 Mapato ya Serikali ........................................................ 7

B.2 Matumizi ya Serikali ..................................................... 12

B.2.1 Matumizi ya Kawaida .................................................. 12

B.2.2 Matumizi ya Maendeleo ............................................... 13

B.2.3 Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati Kwa kipindi cha Julai 2025, hadi Machi 2026 ........................................ 13

C.MWENENDO WA DENI LA TAIFA HADI MACHI 2026 ......... 16

C.1 Mwenendo wa Deni la Taifa ............................................ 16

C.2 Uhimilivu wa Deni la Taifa ............................................ 17

C.3 Dhamana kwa Taasisi za Serikali ................................... 18

D.MISAMAHA YA KODI ........................................................ 19

E.UTEKELEZAJI MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO NA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 - MACHI 2026. ........................................................................ 21

F. UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .......................................... 28

G. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 .................................................... 33

H MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA ............................................................................ 58

H.1 MAPATO .......................................................................... 58

H.1.1 Mapato ya Ndani ......................................................... 58

H.2 MATUMIZI ....................................................................... 61

I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026 ....62
I.1 MALENGO NA SHABAHA ZA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2026 ....................................................62
J. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ...........................64
K. MKAKATI WA SERIKALI KWA MWAKA 2026/2027 ...........78
L. MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ....................................................83
L.1 Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato.............................85
L.1.1 Mapato ya ndani ....................................................85
L.1.2. Mapato yatokanayo na Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ...................................86
L.2 Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi...............................87
M. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2026/2027 ..............88
N. VIPAUMBELE VYA MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027...........................................88
O.MGAWANYO WA SHUGHULI KUU ZA SERIKALI - COFOG.94
P.MAZINGATIO YA MATUMIZI KATIKA MAENEO MAALUM KULINGANA NA SERA ZA MATUMIZI KWA BAJETI YA 2026/2027 ....................................................97
Q. SHUKURANI...................................................100
R.HITIMISHO....................................................108
S.VIAMBATISHO................................................110

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa Kumshukuru Mola wetu Muumba wa vyote vilivyomo Duniani na vile ambavyo viko katika hisia na tusivyo vijua, kwa kutuwezesha kukutana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima na busara katika kutimiza wajibu wetu wa kujadili, kushauri na hatimae kuidhinisha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Serikali.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuendelea mbele naomba kutoa hoja ya kuwa Baraza lako lipokee, lijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

3. **Mheshimiwa Spika,** Uwasilishaji huu unatoa fursa ya kutimiza matakwa ya kifungu cha 105(1 na 2) na kifungu cha 106 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa), na kifungu cha 41(3) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya Mwaka 2016, ambavyo vinamtaka Waziri anayehusika na masuala ya Fedha, kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Serikali kwa Mwaka unaofuata na kuwasilisha Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kwa kuidhinishwa ukiwa na kasma zinazohusisha shughuli mbalimbali zinazohitajika kisheria pamoja na jumla ya fedha zote zinazoombewa kwa Mwaka wa Fedha husika.

4. **Mheshimiwa Spika,** Pongezi za kipekee kwa Jemedari wetu, Mwana Mapinduzi wa Maendeleo na mbunifu wa mageuzi ya kiuchumi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi.** Kwa uongozi wake wenye maono uliowezesha Taifa letu kuendelea kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi. Kwa mara ya kwanza tokea uchaguzi wa vyama vingi vya siasa kufanyika uchaguzi wa kistaarabu na mazingira ya utulivu, hii ni ushahidi wa kukomaa kwa demokrasia yetu na nguvu ya umoja wa wananchi wa Zanzibar. Kwa hakika Historia imeandikwa na vizazi vyetu vitakuja kusimuliwa hadithi yake. Haikuwa rahisi na haikutokea kwa bahati tu, bali ni mipango ya M.Mungu kutokana na Swala, Dua na kariri ya kauli zetu kila kukicha kuzungumzia Amani, Amani, Amani. Hakika Mungu ni mwema amekubali maombi na nia safi daima huwa tabibu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** ameendelea kuwa nguzo imara ya maendeleo ya Taifa kwa kuongoza mageuzi makubwa ya kiuchumi, kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuweka msingi madhubuti wa ustawi wa wananchi na maendeleo endelevu. Hakika morali ya utendaji wake wa kuisimamia Serikali haijawahi kupungua kasi tokea kuingia madarakani. Hali iliyopelekea nasi wasaidizi wake kufanya kazi bila ya kuchoka muda wote ili kukidhi ndoto na dhamira yake ya kuwatumikia wazanzibari.

Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu, amzidishie uwezo, busara na hekima katika kuyadumisha mafanikio hayo kwa manufaa ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa na kipekee, nitoe pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa **Dkt.Samia Suluhu Hassan** kwa imani kubwa aliyoipata kwa Watanzania, kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana. Hakika uongozi wake mahiri, wenye maono na mwelekeo wa kuharakisha maendeleo ya Taifa letu. Chini ya uongozi wake, Tanzania imeendelea kushuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha uchumi, kuendeleza miundombinu ya kimkakati, kuboresha utoaji wa huduma za jamii na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa unaochochea ukuaji wa uchumi jumuishi na ustawi wa wananchi. Aidha, maelekezo yake thabiti kuhusu usimamizi wa fedha za umma, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuendeleza mageuzi ya kiuchumi yameendelea kuweka msingi imara wa utekelezaji wa mipango na vipaumbele vya maendeleo ya Taifa. Busara, maarifa na uzoefu wake umeisaidia sana kuiweka Tanzania salama.

7. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini kwa dhati mchango mkubwa wa Mheshimiwa Rais katika kuendeleza Muungano, kuimarisha ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano na kutoa msukumo wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo yenye manufaa

kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Dira yake ya kujenga Taifa lenye umoja, amani, ustahamilivu na maendeleo endelevu itaendelea kuwa chachu ya kufanikisha azma ya kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

8. **Mheshimiwa Spika,** Sina budi kuwapongeza wasaidizi wake wakuu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa **Dkt. Emmanuel Nchimbi** na Waziri Mkuu Mheshimiwa **Dkt. Mwigulu Lemark Nchemba**. Kwa hakika uongozi wao imara, dhamira yao ya kweli ya kuleta maendeleo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ushirikiano mzuri wanaouendeleza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni wakupigiwa mfano. Sisi upande wa pili wa Muungano tunaendelea kunufaika na ushirikiano na mshikamano uliopo, ambao umeendelea kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

9. **Mheshimiwa Spika,** Mbele ya Baraza lako tukufu, nimesimama kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kuomba ridhaa ya kuidhinishiwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali. Hotuba hii inalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana, kukabiliana na changamoto zilizopo na kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha uchumi wa Zanzibar kwa njia endelevu, sambamba na kuzingatia mwongozo wa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

10. **Mheshimiwa Spika,** Tunafahamu kuwa kwa sasa dunia inaendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi, kupanda kwa gharama za maisha, pamoja na misukosuko ya masoko ya kimataifa. Aidha, migogoro ya kisiasa za Kijiografia (Geopolitics) na kiusalama hususan vita kati ya Marekani, Israili dhidi ya Irani nayo kwa kiasi kikubwa imeathiri nchi zinazoendelea, ikiwemo Zanzibar.

11. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na changamoto hizo, Zanzibar imeendelea kuonesha uimara wa kiuchumi kupitia jitihada za Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuendeleza miundombinu, pamoja na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji. Hatua hizi zimeendelea kuweka msingi imara wa ukuaji wa uchumi endelevu, na kupunguza athari ya moja kwa moja kwa wananchi wa Zanzibar.

12. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kwanza cha awamu ya nane, Serikali imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo inayolenga kuimarisha maisha ya wananchi, ikiwemo sekta za afya, elimu, maji safi na salama, nishati na miundombinu ya usafiri. Mafanikio haya ni ushahidi wa dhamira ya Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ya kuhakikisha maendeleo jumuishi kwa wananchi wote yanafikiwa.

13. **Mheshimiwa Spika,** Bila ya shaka mafanikio hayo, yanatokana na mchango mkubwa wa Kiongozi Mkuu wa

shughuli za Serikali, Makamu wa Pili wa Rais, **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa uongozi wake wenye busara na uzalendo mkubwa katika kuisimamia Serikali yetu. Maelekezo, busara na dhamira yake ya dhati katika kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo yameendelea kuwa nguzo muhimu ya mafanikio ya Serikali. Mchango wake umeendelea kuwa chachu ya mshikamano, uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu, hali inayozidi kuimarisha matumaini ya wananchi wetu na kuharakisha safari ya maendeleo ya taifa letu. Mwenyezi Mungu amuongoze na kumjaalia afya njema katika kuendelea kulitumikia taifa.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa naomba uniruhusu kuwasilisha kwa Muhutasari wa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026.

## B. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI JULAI 2025 – MACHI, 2026

**15.** **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuwasilisha tathmini ya Mapato na Matumizi ya miezi tisa, naomba taarifa za Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar nilizowasilisha asubuhi ya leo wakati wa uwasilishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027, ziwe sehemu ya Hotuba hii.

**B.1 Mapato ya Serikali**

**16.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali ilipanga kukusanya **TZS 6,982.076 bilioni**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2026, Mapato halisi yaliyokusanywa yalifikia **TZS 3,633.87 bilioni** sawa na asilimia 100.34 ya makadirio ya **TZS 3,621.61 bilioni** ya kipindi cha tathmini.

**17.** **Mheshimiwa Spika,** Ongezeko la mapato kwa vyanzo vya Ndani na Nje ni kama ifuatavyo:

- **Mapato ya Kodi** yameongezeka kutoka **TZS 1,142.32 bilioni** hadi **TZS 1,463.43 bilioni** sawa na ukuaji wa asilimia 28, yanayojumuisha:
  a. Mapato kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar ZRA **TZS 826.97 bilioni** sawa na **asilimia 94** ya Makadirio ya kipindi hicho;
  b. Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) upande wa Zanzibar **TZS 620.70 bilioni** sawa na **asilimia 102.11** ya Makadirio ya kipindi hicho; na
  c. Mapato ya Kodi za Wafanyakazi kutoka SMT (PAYE) walioko Zanzibar yalikusanywa kwa asilimia mia moja kama ilivyotarajiwa **TZS 15.75 bilioni**.
- **Mapato Yasiyokuwa ya Kodi** yameongezeka kutoka **TZS 150.15 bilioni** hadi **TZS 167.13 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 11.31 yanayojumuisha:
  a. Mapato ya Wizara **TZS 137.76 bilioni** sawa na **asilimia 75.5** ya Makadirio ya kipindi hicho;
  b. Gawio la Mashirika ya Serikali **TZS 14.94 bilioni** sawa na **asilimia 66.2** ya makadirio; na

c. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, **TZS 14.4 bilioni** sawa na **asilimia 106** ya makadirio.

- **Mikopo ya Ndani** imeongezeka kutoka **TZS 418.47 bilioni** hadi **TZS 1,183.80 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 183, inayojumuisha:

  a. Mikopo ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo **TZS 370.37 bilioni** sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho; na

  b. Mikopo ya Hati Fungani **TZS 813.44 bilioni** sawa na asilimia 103.6 ya makadirio ya kipindi hicho.

- **Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** yameongezeka kutoka **TZS 353.56 bilioni** hadi **TZS 571.74 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 61.71, yakijumuisha:

  a. Misaada **TZS 69.46 bilioni** sawa na asilimia 99 ya makadirio ya kipindi hicho;

  b. Mikopo **TZS 422.30 bilioni** sawa na asilimia 118 ya makadirio ya kipindi hicho;

  c. Misaada ya kibajeti **TZS 79.48 bilioni** sawa na asilimia 127 ya makadirio ya kipindi hicho; na

  d. Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili **TZS 0.51 bilioni** sawa na asilimia 113 ya makadirio ya kipindi hicho.

- **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** yameongezeka kutoka **TZS 10.33 bilioni** hadi **TZS 12.87 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 24.56, na asilimia 95.6 ya Makadirio ya kipindi hicho,

- **Mapato ya Taasisi Zinazojitegemea** kutoka **TZS 129.54 bilioni hadi TZS 234.90 bilioni** sawa na ongezeko la

asilimia 81.34 na asilimia 89.9 ya makadirio ya kipindi hicho.

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini Mapato ya ndani yaliyokusanywa yameonesha ukuaji wa **asilimia 64.5** ukilinganisha na kipindi kama hicho Mwaka 2024/2025, ukuaji huo umetokana na mikakati mbalimbali na hatua zilizochukuliwa na Serikali zikiwemo:

i. Maboresho ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato;
ii. Kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Serikali; na
iii. Kutekeleza sera na hatua za kuimarisha mapato.

### B.1.1 Mapato ya Mfuko wa Miundombinu

19. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026, makusanyo ya kodi ya miundombinu yalifikia **TZS 69.38 bilioni** sawa na asilimi101 ya makadirio ya kukusanya **TZS 68.23 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Kati ya makusanyo hayo **TZS 59.36 bilioni** zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na **TZS 10.02 bilioni** zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar.

### B.1.2 Mapato ya Mfuko wa Barabara

20. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa, Mfuko ulikusanya **TZS 36.30 bilioni** sawa na asilimia 93 ya makadirio ya **TZS 38.98 bilioni** kwa kipindi cha tathmini.

### B.1.3 Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF)

21. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) kwa kipindi cha miezi tisa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umefanikiwa kukusanya **TZS 48.04 bilioni** sawa na asilimia 78% ya lengo la kukusanya **TZS 61.43 bilioni.** Aidha kwa kipindi hicho, ZHSF imepokea jumla ya **TZS 40.15 bilioni** kutoka Serikalini, kwa ajili ya kufanya malipo kwa kampuni za Uwekezaji (Outsources) zinazotoa huduma za afya kwa hospitali za Serikali za Wilaya na Mkoa.

22. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki, Mfuko umetekeleza jukumu lake la msingi kwa kulipa madai ya watoa huduma yenye thamani ya **TZS 12.05 bilioni**, huku ukiimarisha udhibiti wa matumizi kupitia mifumo ya kielektroniki ya uhakiki ambayo inasaidia kupitia madai yasiyo na sifa. Aidha Mfuko umelipa **TZS 28.68 bilioni** kwa kampuni za uwekezaji kwa ajili ya madeni na madai ya wananchi wasiokuwa wanachama wa Mfuko wanaopata huduma katika hospitali za Serikali.

### B.1.4 Kampuni Maalum ya Kisheria (Special Purpose Vehicle)

23. **Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuimarisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Serikali ilianzisha mfumo mbadala wa uwekezaji unaozingatia misingi ya Sharia (Sheria za Kiislamu) unaojulikana kama SUKUK. Hatua hii si tu imepanua wigo wa vyanzo vya fedha, bali pia imefungua milango kwa

wawekezaji mbalimbali kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi imara unaozingatia maadili ya Kiislamu na uwazi.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutenga kiasi cha **TZS 6.5 bilioni** kila mwezi kupitia Mfuko wa miundombinu kwa lengo la kugharamia miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Sukuk. Hadi kufikia Mwezi wa Machi 2026, Serikali imeshatenga jumla ya **TZS 59.58 bilioni** kwa ajili ya kulipia mtaji na faida kwa wawekezaji wa Sukuk. Kwa kipindi cha tathmini Wawekezaji wa Sukuk tayari wameshalipwa jumla ya **TZS 13.03 bilioni** kama nusu ya faida ya mwaka, na nusu ya pili tayari imeshalipwa Mwezi wa Aprili 2026, hivyo kufanya jumla ya malipo kufikia **TZS 26.06 bilioni.**

**25.** **Mheshimiwa Spika**, Wawekezaji hao wamechangia uwekezaji katika miradi ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Unguja (Terminal 2), Ujenzi wa Barabara jumuishi katika Bandari ya Mangapwani, Soko la Samaki Mkoani, Soko la Samaki Fungurefu na Barabara mbali mbali Unguja na Pemba.

**B.1.5 Bima ya Lazima ya Safari kwa Wageni (Mandatory Travel Insurance for Zanzibar)**

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa Bima ya Lazima ya Safari kwa wageni wote wanaoingia nchini, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuimarisha huduma za dharura, kulinda ustawi wa wageni, na kuupunguzia mzigo mfumo wa huduma za afya dhidi ya gharama zisizotarajiwa. Kupitia utaratibu huu, wageni wote wanaoingia nchini

wanatakiwa kuwa na bima itakayogharamia huduma za afya, ajali pamoja na dharura nyingine wanapokaa nchini. Katika kipindi cha tathmini, jumla ya **TZS 76.28 bilioni** zimekusanywa kupitia utekelezaji wa mpango huu. Matumizi hayo yameelekezwa katika maeneo yafuatayo:

i. Mfuko wa Maendeleo ya sekta ya Afya **TZS 27.21 bilioni;**
ii. Bima Mtawanyo **TZS 34.51 bilioni;** na
iii. Gharama za Uendeshaji ni **TZS 14.56 bilioni**.

**B.2 Matumizi ya Serikali**

**27. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa, Serikali ilikadiria kutumia **TZS 3,406.40 bilioni**. Hadi kufikia Machi 31, 2026, kiasi cha **TZS 3,416.30 bilioni** kimetumika, sawa na asilimia **100.29** ya makadirio ya kipindi cha tathmini.

**B.2.1 Matumizi ya Kawaida**

**28. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha tathmini matumizi ya kawaida yalikadiriwa kuwa **TZS 1,694.59 bilioni**, hadi kufikia Machi 31, kiasi cha **TZS 1,646.21 bilioni** kimetumika sawa na ongezeko la asilimia 36.22 ukilinganisha na **TZS 1,208.46 bilioni** zilizotumika katika kipindi kinachofanana kwa Mwaka 2024/2025.

**29. Mheshimiwa Spika,** Matumizi hayo yameelekezwa katika maeneo yafuatayo:

i. Mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zinazo pokea Ruzuku, **TZS 601.78 bilioni;**
ii. Matumizi Mengineyo ya Mafungu na Taasisi za Ruzuku, **TZS 281.56 bilioni;**

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali **TZS 561.58 bilioni;**
iv. Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 10.23 bilioni**; na
v. Matumizi ya Taasisi Zinazojitegemea **TZS 191.05 bilioni.**

**B.2.2 Matumizi ya Maendeleo**

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizotumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo **TZS 1,770.09 bilioni** sawa na asilimia 103 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni:

- Fedha za ndani **TZS 1,414.53 bilioni**;
- Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, **TZS 354.74 bilioni**; na
- Fedha zilizotumika kutekeleza Miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 0.816 bilioni**,

**Kiambatisho Nambari :1** kinahusika

**B.2.3 Utekelezaji wa Maeneo ya Kimkakati Kwa kipindi cha Julai 2025, hadi Machi 2026**

**31.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuharakisha maendeleo ya Taifa, Serikali imejielekeza katika utekelezaji wa maeneo maalum ya kimkakati yenye mchango mkubwa kwa ukuaji wa uchumi, uboreshaji wa huduma za kijamii na kuongeza ustawi wa wananchi, sambamba na kuimarisha ushindani na maendeleo endelevu.

**32. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Kimkakati umefanyika katika maeneo makuu matano (5). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 1,455.549 bilioni** zilipatikana na kutumika katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya kimkakati sawa na asilimia 74 ya makadirio ya **TZS 1,965.434 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:

i. **Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu.** Hadi kufikia Machi 31, 2026, jumla ya **TZS 193.384 bilioni** sawa na asilimia 75 ya lengo la **TZS 256.857 bilioni** zimepatikana na kutumika katika Miradi ifuatayo:

- **TZS 192.978 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba na Bandari Jumuishi–Mangapwani: na
- **TZS 0.406 bilioni** Programu ya kuimarisha maeneo ya kihistoria.

ii. **Mazingira Wezeshi na kuimarisha Miundombinu**. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 678.702 bilioni** sawa na asilimia 94 ya lengo ya TZS 720.853 bilioni zimepatikana na kutumika katika utekelezaji wa miradi ifuatayo:

- **TZS 464.766 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara kuu, Barabara za ndani na Matengenezo ya Barabara za Mjini;
- **TZS 6.474 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Misingi ya Maji, Barabara pamoja na Matengenezo ya Maziwa katika Maeneo ya Mji;

- **TZS 114.514 bilioni** kwa ajili ya Programu ya kuimarisha viwanja vya ndege;
- **TZS 38.716 bilioni** kwa ajili ya Programu ya kuimarisha huduma za usambazaji maji safi na salama Zanzibar; na
- **TZS 54.232 bilioni** kwa ajili ya Programu ya kuimarisha miundombinu ya umeme Zanzibar.

iii**. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi.** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 23.147 bilioni** sawa na asilimia 26 ya lengo la **TZS 89.349 bilioni** zimepatikana na kutumika katika miradi ifuatayo:

- **TZS 17.553 bilioni** Ukarabati wa Maghala, Uhifadhi wa Chakula na Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula;
- **TZS 1.557 bilioni** kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks);
- **TZS 2.946 bilioni** Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar;
- **TZS 1.091 bilioni** Programu ya Mageuzi ya Kidigitali; na

iv**. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii.** Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 439.070 bilioni** sawa na asilimia 59 ya lengo la **TZS 746.185 bilioni** zimepatikana na kutumika katika miradi ifuatayo:

- **TZS199.150 bilioni** Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu;

- **TZS 14.373 bilioni** Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia;
- **TZS 221.676 bilioni** Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo; na
- **TZS 3.871 bilioni** Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia -Binguni.

v. **Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu.** Hadi kufikia Machi 2026, **TZS 121.246 bilioni** sawa na asilimia 80 ya lengo la **TZS 152.189 bilioni** zimepatikana na kutumika katika miradi ifuatayo:

- **TZS 4.833 bilioni** Mradi wa Zanzibar Salama;
- **TZS 108.752 bilioni** Programu ya Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo; na
- **TZS 7.661 bilioni** Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa.

## C. MWENENDO WA DENI LA TAIFA HADI MACHI 2026

### C.1 Mwenendo wa Deni la Taifa

33. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 31, 2026, Deni la Taifa kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limefikia TZS 3,001.63 bilioni. Kati ya Deni hilo TZS 2,987.03 bilioni ni Deni la ndani na TZS 14.6 bilioni ni Deni la nje.

**Deni la ndani limekusanya:**

i. **TZS 1,340.09 bilioni** kutoka benki za biashara na Taasisi za kifedha (PBZ, CRDB, NBC/NMB, STANBIC/ PBZ, ECOBANK, NMB na ZSSF);

ii. **TZS 1,346.59 bilioni** Hatifungani za muda mrefu kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT);

iii. **TZS 300.35 bilioni** ikiwa ni dhamana za Serikali kwa mikopo mbali mbali iliyochukuliwa na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**C.2 Uhimilivu wa Deni la Taifa**

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 31, 2026 thamani halisi ya Deni la Taifa (Ndani na Nje) limefikia **TZS 2,671.03** bilioni, kwa kuzingatia Pato la Taifa (GDP at current prices) la **TZS 6,572.6 bilioni**, ambapo uwiano wa Deni kwa Pato la Taifa limefikia kiwango cha asilimia **40.63**.

**35.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Deni la Taifa lililoripotiwa mwishoni mwa Mwezi wa Machi 2026, limeonesha kuwa ni himilivu kwa kuzingatia uwiano ufuatao:

i. Thamani halisi ya Deni kwa sasa (Face Value) ni **TZS 3,001.63 bilioni;**

ii. Uwiano wa Deni la Taifa kwa ukuaji wa Uchumi kwa thamani halisi kwa kutumia Pato la Taifa GDP “at Constant Price” ya **TZS 7,000.00 bilioni**; na

iii. Uwiano wa Deni la Taifa kwa ukuaji wa uchumi kwa thamani halisi limefikia kiwango cha asilimia **42.88**.

**36.** **Mheshimiwa Spika,** Kiwango cha uwiano kinachokubalika kwa nchi zenye uchumi mdogo au wa kati kama Tanzania inatakiwa kuwa na uwiano wa Deni la Taifa kwa ukuwaji wa uchumi usizidi asilimia **55**.

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Hivyo, hali halisi inaonesha kuwa Deni la Zanzibar bado ni himilivu, ina maana kuwa, Serikali inaweza kuendelea kukopa ili kutekeleza miradi ya maendeleo ya uzalishaji na yenye kuchangia ukuaji wa uchumi.

**C.3 Dhamana kwa Taasisi za Serikali**

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwishoni mwa Machi 2026, Serikali imetoa dhamana zenye thamani ya **TZS 300.345 bilioni** kwa taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo:

i. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati Zanzibar (Zanzibar Utilities Regulatory Authority - ZURA) **TZS 50.000 bilioni;**
ii. Shirika la Meli Zanzibar (Zanzibar Shipping Corporation - SHIPCO) **TZS 69.702 bilioni**;
iii. Shirika la Mawasiliano Zanzibar (Zanzibar Information and Communication Technology Infrastructure Agency – ZICTIA) **TZS 10.000 bilioni**;
iv. Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zanzibar Water Authority - ZAWA) **TZS 65.930 bilioni;**
v. Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (Zanzibar Fisheries Company - ZAFICO) **TZS 28.827 bilioni**;
vi. Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (Zanzibar State Trading Corporation – ZSTC) **TZS 12.907 bilioni**;
vii. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (Zanzibar Airports Authority – ZAA) **TZS 25.594 bilioni**;
viii. Chuo Cha Utawala wa Umma (Institute of Public Administration – IPA) **TZS 3.000 bilioni**;

ix. Shirika la Bima la Zanzibar (Zanzibar Insurance Corporation – ZIC) **TZS 15.000 bilioni;**
x. Kampuni ya Mwani Zanzibar (Zanzibar Seaweed Company Limited – ZASCO) **TZS 2.0 bilioni**;
xi. Wakala wa Uchapaji wa Serikali ya Zanzibar (Zanzibar Government Printing Agency – ZAGPA) **TZS 2.000 bilioni;** na
xii. Manispaa ya Magharibi "A" na "B" **TZS 15.383 bilioni.**

### D. MISAMAHA YA KODI

**39. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, maombi **474** ya misamaha ya kodi kutoka taasisi za umma na binafsi yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, maombi **367** yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya Sheria, na maombi **65** yamekataliwa kutokana na kutokidhi masharti ya Sheria. Aidha, maombi ya misamaha **42** iliyobakia haikukidhi utaratibu wa kuomba misamaha ikiwemo kutokamilika kwa baadhi ya taarifa za maombi.

**40. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko la maombi ya misamaha ya kodi katika vipindi vya tathmini kutoka 294 Mwaka 2024/2025 hadi **474** Mwaka 2025/2026. Aidha, maombi yaliyokubaliwa yameongezeka kutoka 260 Mwaka 2024/2025 hadi **367** katika vipindi vinavyofanana.

**41. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hicho, misamaha yote iliyotolewa ilikuwa na thamani ya jumla ya **TZS 287.814 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 142 ukilinganisha

na **TZS 119.086 bilioni** zilizosamehewa katika kipindi kinachofanana Mwaka 2024/2025, ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA kwa upande wa Zanzibar imetoa misamaha ya **TZS 188.607 bilioni** na Mamlaka ya Mapato Zanzibar-ZRA imesamehe **TZS 99.207 bilioni**.

**42. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo imenufaika kwa asilimia 60.3 ya jumla ya thamani ya misamaha iliyotolewa, miradi ya uwekezaji iliyopitia ZIPA asilimia 32.3, Taasisi za Serikali asilimia 7.2 na asilimia 0.2 Ofisi za Kibalozi na Taasisi za Kidini. Miongoni mwa miradi iliyopatiwa Misamaha ni pamoja na:

i. Mradi wa Bandari Mangapwani;
ii. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Makunduchi;
iii. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Abiria na Mizigo (Zanzibar Passenger and Roro Ferry Terminal);
iv. Mradi wa Uimarishaji na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba;
v. Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Michezo Fumba (AFCON Sport City);
vi. Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tunguu-Makunduchi (48KM) na Fumba- Kisauni (12KM);
vii. Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Beit El Ajaib;na
viii. Mradi wa Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar.

## E. UTEKELEZAJI MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO NA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 - MACHI 2026.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali iliendelea kuchukua na kutekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuongeza uwezo wa kugharamia shughuli za maendeleo na huduma za kijamii. Hatua hizo zilihusu marekebisho ya Sheria pamoja na kuimarisha usimamizi na utawala wa kodi na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:

**Kuimarisha Uzalishaji wa Viwanda vya Ndani**

### E.1 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017

**i. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kwa Uingizaji wa Kuku na Samaki**

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka **TZS 300** hadi **TZS 1,000** kwa uingizaji wa kilo moja ya kuku au samaki. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 3.922 bilioni** zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

### E.2 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015

**i. Kutoza Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Bidhaa**

45. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika ilifanyiwa marekebisho kwa kuweka viwango vya Kodi ya Miundombinu kwa uingizaji wa bidhaa zifuatazo zinazoingia Zanzibar:

a. Lita moja ya maji safi na salama (bottled water) kwa kiwango cha TZS 50;
b. Trea moja ya mayai kwa kiwango cha TZS 1,000;
c. Lita moja ya "soft drink", "carbonated juice" na "non-alcoholic beverage" kwa kiwango cha asilimia tano (5%),
d. Mifuko (Non - Woven Bags) kwa kiwango cha asilimia tano (5%); na
e. Kiwango cha asilimia moja (1%) kwa usafirishaji wa bidhaa nyenginezo.

46. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 3.488 bilioni** zilikusanywa kufuatia utekelezaji wa hatua hii.

**Kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Forodha**

**E.3 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo na Vinywaji Vikali**

47. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa vinywaji vikali (spirit) kutoka TZS 4,386.06 hadi TZS 6,000 na mvinyo (wine) kutoka TZS 4,386.06 hadi TZS 6,000 kwa lita. Kwa kipindi cha Julai 2025, hadi Machi 2026, jumla ya **TZS 1.219 bilioni** zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**ii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Ladha ya Sheesha (Sheesha Flavour)**

48. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka kiwango maalum (specific rate) cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Ladha ya Sheesha (Sheesha Flavour) cha TZS 28,232 kwa kilo moja. Hatua hii imeongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.088 bilion**i.

**iii. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Peremende, Biskuti na Chakileti**

49. **Mheshimiwa Spika**, Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka kiwango cha TZS 1,000 cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Peremende, Biskuti na Chakileti nchini kwa kilo moja ambapo hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 2.193 bilioni** zimekusanywa kutokana na utekezaji wa hatua hii.

**iv. Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Bidhaa za Plastiki (Disposable Items)**

50. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Bidhaa za Plastiki (Disposable Items) kwa kiwango cha 5% kwa kilo moja. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, jumla ya **TZS 0.172 bilioni** zimekusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**v. Kuweka utaratibu wa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa uingizaji wa Gari kubwa zenye uchakavu wa zaidi ya Miaka Mitano**

51. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho na kuanza kutumika Julai 2025, kwa kuweka utaratibu wa kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa gari zenye miaka zaidi ya mitano (5) hadi kumi (10) tokea kutengenezwa kwake kwa kiwango kilichokuwepo sasa cha asilimia kumi na tano (15%). Hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya TZS 0.439 bilioni zilikusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**i. Kuimarisha Ufanisi katika Udhibiti wa Vyombo vya Moto**

### E.4 Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Barabara Nam. 7 ya Mwaka 2003

**i. Kuimarisha Usajili katika Vyombo vya Moto kwa Kuweka Utofauti wa Namba za Usajili**

52. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka Utofauti wa Namba za Usajili kwa vyombo vya maringi manne, matatu na mawili na kuanza kutekelezwa Mwezi Julai, 2025. Hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya vyombo 17,434 vya usafiri wa magurudumu mawili na matatu vimesajiliwa ambapo jumla ya **TZS 0.949 bilioni** zimekusanywa. Aidha, jumla ya magari 23,252 yamesajiliwa kwa kuwekewa utofauti wa namba za usajili ambapo **TZS 1.939 bilioni** zimekusanywa, hatua iliyosaidia kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa mapato yatokanayo na sekta ya usafirishaji.

**ii. Kuanza Rasmi Kusajili Vyombo vya Maringi Manne, Matatu na Mawili Vinavyotumia Nishati ya Umeme Badala ya Nishati ya Mafuta**

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuweka utaratibu wa Kusajili Vyombo vya Maringi Manne, Matatu na Mawili vinavyotumia Nishati ya Umeme Badala ya Nishati ya Mafuta. Aidha, hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya gari kumi na tano (15) zinazotumia nishati ya umeme zilisajiliwa ambapo jumla ya **TZS 0.00195 bilioni** zimekusanywa.

**iii. Marekebisho ya Viwango vya Leseni ya Udereva**

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika ilifanyiwa marekebisho na kuanza kutumika rasmi Mwezi Agosti 2025, kwa kuweka viwango vipya vya ada za leseni ya udereva kama ifuatavyo:

a. Kutoza ada ya TZS 30,000 kwa leseni ya udereva ya mwaka mmoja (1);
b. Kutoza ada ya TZS 45,000 kwa leseni ya udereva ya miaka miwili (2);
c. Kutoza ada ya TZS 60,000 kwa leseni ya udereva ya miaka mitatu (3); na
d. Kutoza ada ya TZS 75,000 kwa leseni ya udereva ya miaka mitano (5).

**55.** Aidha, hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya **TZS 0.270** bilioni zimekusanywa.

### E.5 Marekebisho ya Sheria ya Tozo la Petroli Nam. 8 ya Mwaka 2001

**i. Kuongeza Kiwango cha Leseni ya Barabara na Tozo la Kuendeleza Barabara.**

**56.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho ya viwango vya Leseni ya Barabara na Tozo ya Kuendeleza Barabara (Road Development Fund) kwa kuongeza kiwango cha Leseni ya Barabara kutoka TZS 38 hadi TZS 100, pamoja na kuongeza Tozo la Kuendeleza Barabara kutoka TZS 100 hadi TZS 200 kwa uingizaji wa lita moja ya mafuta ya Dizeli na Petroli. Hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya **TZS 39.328 bilioni** zilikusanywa kutokana na utekelezaji wa hatua hii.

**Kuimarisha Huduma Jumuishi za Kifedha**

**E.5 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

**i. Kutoa Unafuu wa Ushuru wa Bidhaa kwa Taasisi za Fedha wakati Wanaponunua Huduma Kutoka Nje ya Nchi.**

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho na kutekelezwa Julai 2025, kwa kutoa unafuu wa ushuru wa Bidhaa kwa Taasisi za Fedha wakati wanaponunua huduma kutoka Nje ya Nchi.

**Hatua za kuimarisha usimamizi na Utawala wa kodi**

**Kuimarisha ukusanyaji wa Mapato**

**i. Kugomboa Madeni ya Walipa kodi**

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali iliweka utaratibu maalumu wa kugomboa madeni ya kodi, ambapo mlipa kodi atawajibika kulipa kodi stahiki (principal tax) na kusamehe malimbikizo ya adhabu na riba kwa kiwango cha asilimia 100 kwa kipindi

cha miezi sita (6) kuanzia tarehe 1 Julai hadi tarehe 31 Machi 2026, ambapo jumla ya walipa kodi 638 waliwasilisha maombi ya msamaha wa kodi, kati yao 535 kutoka Unguja na 103 kutoka Pemba. Aidha, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya mapato ya **TZS 3.525 bilioni** yalikusanywa, sawa na asilimia 27.65 ya makadirio ya TZS 12.75 bilioni. Hali hii imetokana na mwitikio mdogo wa walipa kodi katika kufanya malipo ya kodi ya msingi pamoja na mwitikio mdogo wa walengwa kuwasilisha maombi ya msamaha wa kodi kwa wakati.

**ii. Kuongeza kiwango cha uthaminishaji kwa uingizaji wa Bidhaa**

59. **Mheshimiwa Spika,** Kuongeza kiwango cha uthaminishaji kwa uingizaji wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango cha sasa. Hatua hii imeongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 19.635 bilioni**.

**iii. Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato yasiyokuwa ya Kodi**

60. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imepewa mamlaka ya kusimamia na kukusanya Mapato Yasiyokuwa ya Kodi. Hadi kufikia Mwezi Machi 2026, jumla ya Taasisi 15 zilianza kusimamiwa na kiasi cha **TZS 78.707 bilioni** kimefanikiwa kukusanywa.

## F. UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2025/2026, tuliainisha hatua kadhaa za kufanya mageuzi mbalimbali ya kisera katika maeneo ambayo yataimarisha ukusanyaji wa mapato na kuimarisha hali ya kiuchumi Zanzibar, maeneo mahsusi ya mazingatio miongoni mwa hayo ni pamoja na:

### F.1 Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Afya

61. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Afya ulipangwa kuiongezea vyanzo vipya vya fedha kwa lengo la kuimarisha sekta ya Afya Zanzibar, na kuwezesha upatikanaji wa huduma ya Afya kwa wote. Hadi kufikia Machi 2026, Mfuko umefanikiwa kuingiziwa **USD 10.4 milioni** sawa na **TZS 27.21 bilioni** kutokana na mgao wa mapato wa Bima ya lazima ya Wasafiri, kati ya hizo USD 6.0 milioni zimetumika katika kuwahudumia wananchi wasiokuwa wanachama wa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar ili kupata huduma bora ya afya katika Hospitali na vituo vya afya vya umma.

### F.2 Soko la Hisa Zanzibar

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imekamilisha upembuzi yakinifu kuhusu uanzishwaji wa Soko la Hisa la Zanzibar, kwa hatua ya awali ripoti iliwasilishwa katika sekretarieti ya kitaalamu ya (IMTC), tumepokea mapendekezo na yameshafanyiwa

kazi na ripoti hio ipo katika hatua ya kuwasilishwa tena Serikalini kwa maamuzi ya mwisho na utekelezaji.

63. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Soko la Hisa linafanikiwa, Serikali imepanga kuweka mifumo imara ya kisheria na kiudhibiti, kuhamasisha ushiriki wa wawekezaji wa ndani, pamoja na utowaji wa elimu ya masoko ya mitaji kwa wananchi na taasisi.

### F.3 Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki kwa ukusanyaji wa Mapato

64. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka Mkakati maalum wa matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwenye Wizara na Taasisi za Serikali, sambamba na kuweka mazingira rafiki kwa wananchi na wafanyabiashara kutumia mifumo ya kielektroniki wakati wanapofanya malipo bila ya kutumia fedha taslimu (cashless economy). Hatua hii imepelekea ukuaji wa mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 64 kwa kipindi cha tathmini kutoka **TZS 1,710.94 bilioni** hadi kufikia **TZS 2,813.96 bilioni.**

### F.4 Benki ya Uwekezaji Zanzibar (Zanzibar Investment Bank)

65. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeshachukua hatua kadhaa juu ya uanzishaji wa Benki ya Uwekezaji ambayo itasaidia kuimarisha upatikanaji wa mitaji na huduma za kifedha kwa ajili ya kuchochea uwekezaji, ukuaji wa sekta binafsi pamoja na maendeleo endelevu ya uchumi wa Zanzibar, kwa sasa tayari tumeingia mkataba na Mshauri Elekezi

(Ernest & Young) kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji Zanzibar (Zanzibar Investment Bank). Hatua iliyofikia kwa sasa Mshauri Elekezi (Ernest & Young) amewasilisha Ripoti ya Awali (Interim Report) pamoja na kuendelea na hatua ya kukusanya maoni ya wadau kwa upande wa Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwasilisha ripoti ya mwisho.

### F.5 Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo Kupitia Green House na Uimarishaji wa Zao la Karafuu

66. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeongeza jitihada katika kusimamia uzalishaji na uuzaji wa karafuu ambapo, kiasi cha **TZS 83.9 bilioni** zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa **tani 5,616** za karafuu kavu kutoka kwa wakulima na **TZS 1.57 bilioni** kwa ajili ya ununuzi wa tani 793 za makonyo. Ili kuondosha usumbufu wa uuzaji na ununuaji wa karafuu, Serikali imeongeza juhudi kwa kujenga kituo kipya cha uuzaji na ununuzi wa karafuu katika eneo la Kiwani Pemba, sambamba na kufanya matengenezo makubwa ya vituo saba vya ununuzi wa karafuu.

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kilimo cha green house kwa lengo la kuongeza tija, kuimarisha uzalishaji wa mazao yenye ubora na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

68. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya Green House 3 zilijengwa Matemwe Wilaya ya Kaskazini ‘B’ zikiwa na mfumo wa nguvu za jua ‘Solar System’, zenye ukubwa wa 8m kwa

15m, na ziligharimu kiasi cha **TZS 40 milioni**. Wanufaika wa vikundi vitatu vya ushirika ambavyo vinajishughulisha na uzalishaji wa mboga walipatiwa mafunzo, mashamba darasa, na mifumo ya umwagiliaji wa matone.

### F.5 Utekelezaji wa Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa

**69. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali ilitenga **TZS 71.926 bilioni** kwa Wizara nane za majaribio kwa ajili ya kutekeleza shughuli zinazohusiana na masuala ya jinsia na usawa, hadi kufikia Machi 31,2026 kiasi cha **TZS 22.131 bilioni** ya fedha zilizopangwa zimepatikana na kutumika.

**70. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa bajeti inayozingatia Jinsia na Usawa ni moja kati ya kipaumbele cha Serikali kwa lengo la kuhakikisha rasilimali fedha zinaelekezwa katika jamii kwa kuzingatia mahitaji halisi ya makundi yote wakiwemo wanawake, wanaume, wasichana, vijana, wazee, watu wenye mahitaji maalum na watoto. Katika kipindi cha tathmini, miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuwapatia Mafunzo ya muda mrefu madaktari bingwa 237 (wanawake 131 na wanaume 106) katika kada mbalimbali zikiwemo za Afya ya Uzazi na Watoto;
ii. Kuwapatia mikopo nafuu watu wenye ulemavu kupitia programu ya 4:4:2. ambapo wanufaika 1,073, walipatiwa mkopo huo (wanaume 72 na wanawake ni 1,001);

iii. Kufanya mafunzo ya uongozi na usimamizi kwa wanawake katika sekta ya uvuvi;
iv. Kupatiwa mafunzo ya uendeshaji wa mabonde yote ya Umwagiliaji, ambapo jumla ya wakulima 1,359 (662 wanawake na 697 wanaume) walinufaika;
v. Kuandaa muongozo wa mpango mkakati wa kijinsia unaojumuisha shughuli zote za Mahkama sambamba na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha utekelezaji wenye tija;
vi. Utoaji wa haki kwa kuzingatia jinsia wananchi 13,364 walinufaika na huduma zilizotolewa kati yao wanawake walikuwa 8,008 (60%) na wanaume 5,356 (40%);
vii. Kufanya ufuatiliaji wa skuli 73 (54 za msingi na 19 za sekondari) kwa Watoto wenye mahitaji maalum sambamba na kutoa mafunzo kwa wajumbe 120 wa timu za wataalamu kuhusu matumizi ya vifaa vya upimaji kabla ya watoto kuanza skuli;
viii Kuhamasisha vijana wanawake 250 juu ya matumizi ya mbinu bora za kilimo cha mboga mboga na kuwasaidia vifaa vya kilimo, pamoja na kutoa mafunzo kwa vijana wanawake 282 juu ya kilimo biashara; na
ix. Uchapishaji, uandishi na usambazaji wa muongozo wa hukumu kwa lugha nyepesi juu ya uchunguzi, mashtaka na uamuzi wa kesi za ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto Zanzibar.

## G. MAFANIKIO YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha pili cha Serikali ya awamu ya nane, Serikali imeendelea na jitihada za kutekeleza Miradi katika nyanja na hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha utekelezaji wa **Bajeti yenye kuzingatia matokeo** (Program Based Budget -PBB).

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba nieleze kwa muhutasari miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ambayo yanaonesha dhamira ya Serikali ya kuendelea kujenga mfumo imara, endelevu na shindani kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla kupitia utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026:

**a. Ukuaji wa Mapato Halisi ya Serikali**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini, mapato halisi ya Serikali yameongezeka kutoka **TZS 2,204.37 bilioni** hadi kufikia **TZS 3,633.48 bilioni** sawa na ongezeko la ukuwaji wa asilimia **64.85**;

**b. Uimarishaji wa Miundombinu ya usafiri**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri ikiwemo Ujenzi na Matengenezo ya Barabara, Viwanja vya Ndege na Bandari katika maeneo mbalimbali nchini. Hatua hiyo imeongeza ufanisi wa usafirishaji na usafiri, kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na kuimarisha mtandao wa mawasiliano.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa, Serikali imetumia kiasi cha **TZS 850.857 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Ujenzi na matengenezo ya Miundombinu ya Barabara, Programu ya kuimarisha Viwanja vya Ndege na Programu ya kuimarisha bandari. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na:

- **Usafiri wa Baharini,** Serikali imetumia jumla ya **TZS 123.517 bilioni,** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, Ujenzi wa Bandari ya Abiria na Mizigo Mpiga Duri, Ujenzi wa Bandari kavu ya Maruhubi na Ujenzi wa boti mbili za abiria za mwendokasi;
- **Usafiri wa Anga,** Kiasi cha **TZS 71.715 bilioni** zimetumika kwa ajili ya kuimarisha ujenzi wa viwanja vya Ndege Pemba, na kukamilisha ujenzi wa Jengo jipya la Pili la Abiria (Terminal II) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume; na
- **Usafiri wa Nchi Kavu (Barabara), TZS 699.473 bilioni**, zimetumika katika kukamilisha ujenzi wa barabara zenye jumla ya **kilomita 240.7** kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba, pamoja na kuendelea na ujenzi wa misingi ya kuondolea maji ya mvua yaliyotuwama katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar.

**c. Kuimarika kwa Huduma za Kijamii**

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea kujenga ustawi wa wananchi, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za kijamii kwa kuzingatia upatikanaji wa huduma bora,

jumuishi na endelevu katika sekta za afya, elimu, maji ,umeme na ustawi wa jamii.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Tathmini Serikali imetumia jumla ya **TZS 375.036 bilioni** kwa ajili ya kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo:

- **Miundombinu ya Elimu**

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya elimu kupitia ujenzi na ukarabati wa madarasa, maabara, dakhalia na nyumba za walimu katika maeneo mbalimbali nchini. Hatua hiyo imeongeza mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia, kupunguza msongamano wa wanafunzi pamoja na kuimarisha ubora wa elimu.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji huo unaendelea kuakisi dhamira ya Serikali ya kuendeleza na kuwekeza katika rasilimali watu kupitia sekta ya elimu kama msingi muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **TZS 221.489 bilioni** zimetumika kwa ajili ya Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu, ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia pamoja na mkopo wa elimu ya juu.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Shughuli nyengine zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. **Kuimarisha Elimu ya Sekondari,** Kiasi cha **TZS 306.480 bilioni** zilitumika kwa ajili ya kuanza ujenzi wa skuli saba za ghorofa zenye madarasa 179 Unguja na Pemba na kukamilisha skuli mpya 13;

ii. **Elimu ya Maandalizi na Msingi,** Serikali imetumia **TZS 250.051 bilioni** kwa ajili ya ujenzi wa skuli za ghorofa nane za msingi zenye madarasa 256 pamoja na kukamilisha skuli 21 mpya Unguja na Pemba;

iii. **Kuimarisha Elimu ya juu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**. Serikali imetumia **TZS 175.836 bilioni** kwa ajili ya kuimarisha Elimu ya juu na kuendeleza taaluma za kisasa zikiwemo Artificial Intelligence, Data Science na Aquaculture sambamba na elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu;

iv. **Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali,** kiasi cha **TZS 36.651 bilioni** zimetumika kwa lengo la kuwajengea vijana ujuzi wa kujiajiri na ushindani katika soko la ajira; na

v. **Kuongeza Fursa za Mikopo ya Elimu ya Juu TZS 37.945 bilioni** kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu ambapo wanafunzi 18,593 wamenufaika, wakiwemo wanafunzi wapya 8,975 na wanafunzi 9,618 wanaoendelea na masomo ndani na nje ya nchi. Aidha, wanafunzi 335 wamepatiwa ufadhili maalum wa masomo kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi washirika.

- **Uimarishaji wa huduma za Afya**

**81. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Afya ni sekta mtambuka. Serikali imekuwa ikiweka jicho lake muda wote ili kuhakikisha ustawi wa wananchi na kuongeza tija katika maendeleo ya Taifa, miundombinu na vifaa tiba vinaimarika, upatikanaji wa huduma bora za afya pamoja na kuongeza

upatikanaji wa wataalamu na dawa muhimu, Hadi kufikia Machi 2026 kiasi cha **TZS 64.549 bilioni** zimetumika kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo:

i. Programu ya kuimarisha miundombinu ya afya, ujenzi wa Hospitali, Vituo vya afya ya msingi, Nyumba za wafanyakazi pamoja na ununuzi wa vifaa tiba **TZS 53.202 bilioni;** na

ii. Proramu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza **TZS 11.347 bilioni.**

- **Upatikanaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama**

**82. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikichukua hatua za makusudi kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wetu, maeneo ambayo yamekuwa yakiimarishwa ni pamoja na kuendeleza miundombinu ya maji, kuongeza usambazaji wa huduma vijijini na mijini, pamoja na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2025 hadi Machi 2026, kiasi cha **TZS 29.116 bilioni** kimetumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar ikiwemo:

i. Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar **TZS 14.268 bilioni**; na

ii. Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar **TZS 14.848 bilioni.**

83. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kukamilisha Mradi wa Ukarabati wa Miundombinu ya Maji Kengeja-Pemba, ikiwemo ukarabati wa tangi la maji la lita 300,000, uchimbaji wa kisima kipya na ulazaji wa mtandao wa mabomba kilomita 13.7, nyumba 1,850 zimeunganishwa kwa kupatiwa huduma ya maji safi na salama, katika Shehia ya Kengeja, Chole na Vijiji Jirani.

- **Sekta ya Nishati na Umeme**

84. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweka kipaumbele kikubwa katika kuimarisha Sekta ya Nishati na Umeme kwa kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya uhakika, endelevu na gharama nafuu kupitia uwekezaji wa kimkakati katika uzalishaji na usambazaji wa umeme, ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kuchochea kasi ya maendeleo ya uchumi wa Taifa, hususan katika maendeleo ya viwanda, biashara, uwekezaji na ustawi wa wananchi.

85. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **TZS 54.232 bilioni** zimetumika kutekeleza Programu ya kuimarisha miundombinu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar. Serikali imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kupanua mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha 33kV na 11kV. Jumla ya urefu wa kilomita 48.96 wa mtandao wa kusafirisha umeme umejengwa sawa na asilimia 142 ya mpango uliowekwa wa kujengwa kilomita 34.5 katika kipindi hicho. Aidha, kwa upande wa mtandao wa umeme mdogo, Serikali imefanikiwa kujenga kilomita 225.75 kwa

kipindi cha Julai - Machi, 2025/2026, sawa na asilimia 272 ya mpango uliowekwa wa kujengwa kilomita 83 katika kipindi hicho.

86. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imeendelea kuandika historia ya mafanikio makubwa katika sekta ya nishati kwa kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za mafuta na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa bidhaa ya mafuta nchini. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kuwasili kwa mara ya kwanza kwa meli ya mafuta ya MT CLEAROCEAN MIRACLE katika Bandari ya Mangapwani Zanzibar, tukio hilo la kihistoria linaloashiria hatua mpya ya maendeleo ya miundombinu ya nishati na uwezo wa nchi katika kupokea na kuhifadhi bidhaa za mafuta moja kwa moja.

87. **Mheshimiwa Spika,** Meli hiyo ilileta jumla ya lita 36,271,100 za bidhaa za mafuta, zikiwemo lita 14,702,045 za petroli, lita 11,476,392 za dizeli na lita 10,092,663 za mafuta ya ndege. Mafanikio haya yamepunguza changamoto za usafirishaji na usambazaji wa mafuta kupitia njia mbadala, pamoja na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa nishati. Hatua hii ni dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya kimkakati ya nishati.

**d. Uimarishaji wa Ulinzi na Usalama**

88. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama nchini kwa kuongeza uwezo wa vyombo vya ulinzi na usalama, matumizi ya teknolojia pamoja na kuimarisha mifumo ya kiintelijensia. Mafanikio hayo

yameendelea kudumisha amani, utulivu na mazingira salama ya utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi nchini. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **TZS 59.758 bilioni** zimetumika zikiwemo:

i. **TZS 43.747 bilioni** kwa ajili ya Mradi wa uimarishaji wa ulinzi na usalama; na

ii. **TZS 16.181 bilioni** kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi na uboreshaji wa Mahkama za Mikoa.

**e. Maendeleo ya Sekta ya Fedha**

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya fedha ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta hii inajumuisha huduma za Benki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Soko la Mitaji na Dhamana, Mifumo ya malipo na huduma ndogo za fedha (Microfinance).

- **Sekta Ndogo ya Benki**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta hii inajumuisha; Benki za biashara, Mawakala wa huduma za kibenki na mitandao ya simu. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, sekta hii iliendelea kuimarika kutokana na kukua kwa teknolojia, utumiaji wa njia mbadala wa kufikisha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na mawakala wa benki (banking agents). Kwa kipindi cha tathmini, sekta hii imechangia wastani wa asilimia **5.4** katika ukuaji wa pato la Taifa la Zanzibar. Aidha idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma zimeongezeka na kufikia 16, huku idadi ya matawi ya benki yamefikia 58 (Pemba 20 na Unguja 38).

- **Amana**

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2025, amana katika benki zilizopo ziliongezeka kwa asilimia 22.8 kutoka **TZS 3,021 bilioni** hadi kufikia **TZS 3,711 bilioni** kwa kipindi cha tathmini. Benki ya Watu ya Zanzibar (PBZ) ilikuwa na asilimia 51.0 ya amana zote; ikifuatiwa na benki ya CRDB asilimia 12.7, NMB asilimia 10.8, NBC asilimia 8.4, na bakaa ilikuwa kwa benki nyingine za biashara zilichangia asilimia 17.1 ya amana zote hapa Zanzibar.

- **Wakala wa Huduma za Kibenki**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Machi 2026, idadi ya mawakala wa benki (banking agents) waliongezeka na kufikia **8,597** sawa na ongezeko la asilimia 4.6 ya mawakala wote nchini Tanzania kutoka **6,379** waliokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2024. Pemba kulikuwa na mawakala 4,462 na Unguja mawakala 4,135.

- **Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Rate Movement)**.

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani. Kwa wastani, shilingi ilibadilika hadi kufikia TZS 2,559.80 kwa dola, ikilinganishwa na TZS 2,613.68 katika kipindi kama hicho Mwaka 2025.

- **Huduma za Bima Zanzibar**

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Hali ya Soko la Bima kwa upande wa Zanzibar inazidi kuimarika. Biashara ya Bima imekuwa kwa asilimia 222% ambapo kukua huko kumesababishwa na:

i. Kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha bidhaa zinazounda kundi la Bima nyinginezo ikiwemo Bima za Miamala ya Fedha (Money Insurance), Bima ya Wasafiri wanaoingia nchini (Inbound Travelling Insurance), Bima za Wizi, Fidia kwa Wafanyakazi (Worksman Compensation) na Hati Fungani;

ii. Utekelezaji wa bima ya wageni wanaoingia nchini kama hatua ya kimkakati ya kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar;

iii. Kuimarika kwa huduma za takaful;

iv. Kuimarishwa kwa ushirikiano wa taasisi (inter-agency coordination) kwenye utekelezaji wa bima za lazima;

v. Kuwa na mashirikiano ya kimfumo na ZRA na Jeshi la Polisi Zanzibar;

vi. Kufungua Ofisi za Kanda za Unguja na Pemba;

vii. Matumizi ya bima kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulinda majengo ya Umma, gari za Serikali, Bima ya Afya na Miradi ya maendeleo;

viii. Kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Kampuni na Benki mbalimbali katika mfumo wa (Bancassurance) kama vile (VodaBima, Zanztel Yas Bima, Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, Equity Bank, MUKOBA Bank na PBZ Bank);

ix. Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Madai (Digital Claims Management System); na

x. Kuanzishwa kwa Programu ya Bima kiganjani (ZIC Bima App) ambayo inamuwezesha mteja kununua bima moja kwa moja kwa kutumia simu na kufanya malipo kwa njia ya kidijitali.

- **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar**

**95. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umeendelea kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii, kuongeza uwezo wa kifedha wa Mfuko pamoja na kutekeleza Miradi ya Maendeleo yenye tija kwa wananchi. Miongoni mwa Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji wa Mfuko kutoka **TZS 1.165 trilioni** kwa mwaka 2025 hadi **TZS 1.481 trilioni** mwaka 2026, sawa na ongezeko la asilimia **27** kwa kipindi cha tathmini;

ii. Kuongezeka mapato ya uwekezaji na mapato mengineyo kutoka **TZS 85.50 bilioni** hadi kufikia **TZS 204.92 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia 140 kwa kipindi cha tathmini;

iii. Michango ya wanachama kutoka **TZS 117.18 bilioni,** hadi kufikia **TZS 135.90 bilioni** sawa na ongezeko la asilimia **16** kwa kipindi cha tathmini;

iv. Kulipwa kwa mafao mbalimbali kwa wanachama na wastaafu yenye thamani ya **TZS 69.18 bilioni** katika kipindi hicho;

v. Kulipwa kwa pencheni kwa wastaafu **14,335** kwa thamani ya **TZS 32.27 bilioni** kwa kipindi cha tathmini; na

vi. Kukamilika kwa asilimia 100 kwa Mradi wa Kituo cha Kisasa cha Mabasi Malindi, Soko la Mombasa pamoja na Nyumba za Gharama Nafuu eneo la Mombasa Zanzibar sambamba na kuanza taratibu za ujenzi wa kituo cha mabasi Jumbi na Koani.

- **Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu kwa Mfumo wa IPSAS Accrual**

**96. Mheshimiwa Spika,** Serikali ipo katika hatua za kuhama katika kufunga hesabu za Serikali kwa kutumia viwango vya kimaifa vya uhasibu kwa sekta za umma taslimu (IPSAS cash), kuelekea viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma halisi (IPSAS accrual), kwa lengo la kuimarisha uwazi, uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma sambamba na kuongeza ubora wa taarifa za kifedha za Serikali. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kiasi cha **TZS 0.564 bilioni** zimetumika. Hali hii itasaidia Serikali kuweza kutambua hali halisi ya mali na madeni. Uhamiaji huu utaanza kufanyiwa kazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**f. Uendeshaji wa Mashirika ya umma**

**97. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025, hadi Machi 2026, uendeshaji wa Mashirika ya Umma umeendelea kuimarika kupitia usimamizi mzuri wa shughuli za kila siku, utekelezaji wa mipango ya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuimarika kwa usimamizi wa mapato yanayotokana na ukusanyaji wa gawio na michango kutoka katika Mashirika ya Umma. **TZS 14.95 bilioni** zimekusanywa sawa na ongezeko la asilimia **76** kutoka **TZS 8.5 bilioni** zilizokusanywa kipindi kama hichi mwaka uliopita; na
ii. Kuongezeka kwa uwajibikaji wa Mashirika ya Umma kupitia kufunga mikataba ya utendaji kazi pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mikataba hiyo. Hatua hiyo imeiwezesha Serikali kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma na usimamizi wa rasilimali za umma kwa mashirika husika.

**g. Mashirikiano ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miezi tisa, Serikali inaendelea kuimarisha mashirikiano ya kimataifa na kitaifa kama nyenzo muhimu ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kidiplomasia. Katika kipindi hiki, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alitembelewa na Mabalozi, Mawaziri, Wawekezaji pamoja na wageni mashuhuri wa kimataifa waliowakilisha nchi na taasisi mbalimbali duniani.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Ziara hizi za wageni zimedhihirisha kuimarika kwa hadhi ya Zanzibar katika medani ya kimataifa pamoja na kuongezeka kwa imani ya jumuiya za kimataifa juu ya mazingira mazuri ya uwekezaji, diplomasia na maendeleo yaliyopo nchini. Mazungumzo yaliyofanyika kati ya Mheshimiwa Rais na viongozi hao yalizaa mafanikio muhimu katika maeneo manne ya kimkakati:

i. **Kuimarisha ushirikiano, fursa za uwekezaji,** kupitia Kaimu Balozi wa Marekani, Balozi Andrew Lentz miradi iliyo jadiliwa katika uwekezaji huo ni; Bandari ya Mangapwani, umeme, hifadhi ya mafuta, afya na mabadiliko ya tabianchi;

ii. **Ushirikiano wa kidini,** Serikali inaendelea kunufaika na fursa za kimataifa katika masuala ya dini kupitia ushirikiano wa kimkakati uliofanyika kati ya Serikali na Waziri wa Hijja na Umrah wa Saudi Arabia, Mhe. Tawfiq bin Fawzan Al-Rabiah & Balozi wa Saudi Arabia, Mhe. Yahya bin Ahmed Okeish, kwa kuunga mkono Mfuko wa Hijja wa Zanzibar, elimu ya Kiislamu, na kuongeza safari za ndege kipindi cha Hijja;

iii. **Sekta ya utalii,** Kupitia Waziri wa Mambo ya Kale na Utalii wa Oman, Mhe. Sheikh Salim bin Mohammed Al Mahrouqi & Balozi Mdogo wa Oman, maeneo yaliyo jadiliwa kuimarishwa ni pamoja na; Uhusiano wa kihistoria, utalii, utamaduni, na ukarabati wa majengo ya kihistoria kama Beit al Ajaib, Mtoni Palace na uhifadhi wa urithi wa Mji Mkongwe. Aidha, ujio wa viongozi wa mashindano ya kimataifa ya Miss World uliitangaza Zanzibar katika majukwaa ya kimataifa na kuongeza fursa za kuitangaza kama kitovu cha utalii, uwekezaji na huduma za kimataifa; na

iv. **Sekta ya afya na maendeleo ya teknolojia,** majadiliano hayo yaliwezesha kupatikana kwa fursa muhimu za ushirikiano katika utoaji wa huduma za matibabu ya

kibingwa. Ushirikiano huo unahusisha kwa kiasi kikubwa huduma za upasuaji wa mishipa ya fahamu, pamoja na maeneo mengine ya tiba maalumu yanayohitaji utaalamu wa hali ya juu.

100. **Mheshimiwa Spika,** Maeneo mengine ambayo Serikali imenufaika ni ubadilishanaji wa uzoefu na teknolojia, kuendeleza diplomasia ya uchumi kupitia:

i Kuratibu ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya jumuiya za kikanda na ushirikiano wa kimataifa (EAC, SADC, AfCFTA, IORA) ili kuimarisha utatuzi wa changamoto mbalimbali na kuongeza upatikanaji wa fursa za maendeleo kwa Zanzibar;

ii Kushiriki mikutano 17 ya Jumuiya za Kikanda za EAC, SADC na AfCFTA ndani na nje ya nchi, hatua iliyochangia kuongeza fursa za maendeleo na kuwajengea uwezo wadau katika kukuza sekta muhimu za uchumi ikiwemo Uchumi wa Buluu, Uwekezaji, Biashara na Ujasiriamali. Ushiriki huo umeiwezesha Zanzibar kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi na maendeleo;

iii Mfumo rasmi wa Usajili wa Diaspora wa Zanzibar umeanza kutumika unaoiwezesha Serikali kupata takwimu halisi za Diaspora wa Zanzibar ikiwemo nchi wanazoishi, taaluma na ujuzi, biashara na uwekezaji kwa lengo la kushirikiana katika masuala ya uchumi, fursa na maendeleo; na

iv Serikali pia, ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 552.46 Milioni** kutoka Diaspora wa Zanzibar Duniani ambapo zaidi ya familia 1,200, watoto 382 na wanafunzi 18 wa Chuo cha Mafunzo walioachiwa huru walifaidika na misaada, sadaka na fidia zilizotolewa kwa kipindi hiki.

**h.Ushiriki wa Shughuli za Kijamii na Kidini**

**101. Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameendelea kutoa kipaumbele katika kushiriki na kuunga mkono shughuli mbalimbali za dini na kijamii kama sehemu ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa, maadili na ustawi wa jamii. Ushiriki wake katika shughuli hizo umeendelea kudhihirisha dhamira ya Serikali ya kudumisha umoja, amani, upendo na mshikamano miongoni mwa wananchi, sambamba na kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Taifa.

**102. Mheshimiwa Spika,** Kwa mara ya kwanza Zanzibar iliandika historia kupitia futari ya Kitaifa iliyowaunganisha wananchi kutoka makundi mbalimbali ya kijamii pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Tukio hilo lilikuwa ishara ya kuimarisha mshikamano wa kitaifa, kuendeleza maadili ya umoja, upendo na ushirikiano miongoni mwa wananchi, sambamba na kudumisha utamaduni wa Kizanzibari wa kufutari pamoja. Kwa mujibu wa takwimu waumini wapatao 27,345 walihudhuria katika futari hiyo iliyofanyika katika Uwanja wa ***New Amaan Complex***.

### i. Mashirikiano na Washirika wa Maendeleo

103. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuvutia fursa za uwekezaji kupitia mikutano na mabalozi pamoja na wajumbe kutoka nchi mbalimbali ikiwemo; Umoja wa Ulaya, Ujerumani, Saudi Arabia, Oman, India, Canada na Brazil, hatua iliyolenga kukuza sekta za utalii, afya, elimu, biashara, miundombinu na uchumi wa buluu. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali imefanikisha mambo yafuatayo:

i Utiaji wa saini wa Mikataba miwili ya Ruzuku yenye thamani ya NOK 43.9 million sawa na TZS 12.4 billion kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Sustainable Energy Supply, Use and Management in Zanzibar kutoka Serikali ya Norway na Mkataba wa ruzuku wa USD 6.2 million sawa na TZS 16.2 bilioni kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya uhifadhi wa misitu na utunzaji wa mazingira ya ukanda wa Bahari Zanzibar [Safeguarding Zanzibar's Forest and Coastal Habitats for Multiple Benefits];

ii Kushiriki katika mikutano ya kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa la [IMF], na kufanya majadiliano yaliyoratibiwa na Wizara ya Fedha ya Tanzania juu ya Miradi ya kipaumbele inayotarajia kupata nyongeza ya fedha ambayo ni; Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto **USD 100 million** sawa na TZS 260.00 bilioni, Mradi wa kuifanyia mabadiliko Sekta ya Nishati-ZESTA **USD 107.19 million**

sawa na TZS 278,69 bilioni na Programu ya kuboresha Elimu ya Sekondari Zanzibar Improving Quality of Basic Education Project **USD 40 million** sawa na TZS 104.00 bilioni;

iii Kuidhinishwa kwa Mradi wa Tanzania Scaling-up Sustainable Marine Fisheries and Aquaculture Management Project, [TASFAM] jumla ya **USD 117 milioni**, kati ya fedha hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kupata **USD 41 milioni** sawa na TZS 106.60 bilioni kupitia Benki ya Dunia;

iv Kudhinishwa kwa mradi wa Submarine Cable na **USD 282.5 million** sawa na TZS 734,50 bilioni kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);

v Kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watendaji wa Serikali 310 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China MOFCOM PROGRAM na Benki ya Maendeleo ya Uchumi Afrika (BADEA); na

vi Kuratibu upatikanaji wa Msaada wa kiufundi kutoka katika kituo cha Sheria (Afrika Legal Support Facility (ALSF)) kilichopo chini ya Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa lengo la kujengewa uwezo juu ya usimamizi wa mikataba na Deni la Taifa.

**j. Uwekezaji**

**104. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji kupitia sera, sheria na miundombinu wezeshi kwa lengo la kuvutia mitaji na kuongeza shughuli za

uzalishaji nchini. Hatua hizo zimechangia kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuimarisha mapato ya Taifa.

105. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026, Serikali imesajili miradi ya uwekezaji **104** yenye thamani ya dola za kimarekani **676** Milioni katika sekta ya Utalii, Real Estate, Viwanda na Mifugo.

106. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha tathmini Miradi **17** imefunguliwa yenye mtaji wa thamani ya **USD 243.8 milioni** na kutoa ajira 1,567, miongoni mwa miradi hio ni:

i Mradi wa Zanbreed wenye mtaji wa USD 105 milioni na kutoa ajira zipatazo 1,000;

ii Mradi wa Jaz Elite Aurora wenye mtaji wa USD 100 milioni na kutoa ajira zipatazo 200; na

iii Mradi wa Matemwe Bangalow umewekeza jumla ya **USD 22 milioni** na kutoa ajira 197.

k**. Utekelezaji wa Miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP),**

107. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kupitia uratibu wa miradi 6 ya ubia (PPP) yenye thamani ya zaidi ya **TZS bilioni 752.7** katika sekta mbalimbali ikiwemo michezo, usafiri wa anga, maeneo ya kihistoria pamoja na huduma za jamii. Hatua hiyo imeongeza thamani ya miradi ya PPP nchini kufikia Dola za Kimarekani **bilioni 1.2** na hivyo kuendelea kuimarisha mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya Taifa.

### l. Uchumi wa Buluu

108. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea kutekeleza dira ya maendeleo endelevu kupitia Uchumi wa Buluu, Serikali imepata mafanikio makubwa katika kuimarisha matumizi ya rasilimali za bahari kwa ajili ya kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuimarisha ustawi wa wananchi. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **TZS 37.079 bilioni** zimetumika kutekeleza:

i Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki **TZS 8.614 bilioni;**

ii Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) **TZS 9.512 bilioni;**

iii Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini **TZS 2.685 bilioni**; na

iv Usimamizi wa Uvuvi Endelevu na utafiti wa usalama wa chakula kwa Viumbe Maji wa Bahari **TZS 16.268 bilioni.**

### m. Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale

109. **Mheshimiwa Spika** Serikali imetumia jitihada za makusudi ili kuendeleza vivutio vya utalii, kuhifadhi urithi wa kihistoria na utamaduni, pamoja na kuboresha huduma na miundombinu ya utalii, ili kuongeza idadi ya watalii, mapato ya fedha za kigeni. Hadi kufikia machi 2026 kiasi cha **TZS 0.406 bilioni** kimetumika kwa ajili ya Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria.

### n. Biashara na Viwanda

110. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inandelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji, kuhamasisha uzalishaji wa viwandani na kuendeleza biashara za ndani na nje ya nchi. Hatua hizo zimechangia kuongeza ajira, thamani ya uzalishaji pamoja na kukuza uchumi wa Taifa. Kwa kipindi cha tathmini kiasi cha **TZS 1.557 bilioni** zimetumika kwa ajili ya kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks).

### o. Sekta ya Kilimo

111. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza ajira na kuongeza tija katika kilimo, Serikali inaendelea kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji, huduma za upatikanaji wa pembejeo na masoko kwa lengo la kuchochea ukuaji wa Uchumi kwa mtu mmoja mmoja.

112. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025, hadi Machi 2026, kiasi cha **TZS 39.663 bilioni** zimetumika kwa ajili ya kutekeleza maeneo yafuatayo:

i Kuimarisha mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na uzalishaji kupitia huduma za kisasa **TZS 33.113 bilioni**

ii Kuendeleza miundombinu ya mifugo na misitu **TZS 0.143 bilioni;**

iii Programu ya ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji **TZS 4.035 bilioni**; na

iv Mageuzi ya uzalishaji wa Maziwa kwa wafugaji wadogo unaozingatia mabadiliko ya tabianchi **TZS 2.273 bilioni.**

### p.Maendeleo ya Habari, Utamaduni na Michezo

**113.** **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Habari, Utamaduni na Michezo ni moja ya eneo la kuimarisha mifumo ya upashanaji habari, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Taifa, pamoja na kuimarisha michezo na vipaji vya vijana ili kukuza uzalendo, ajira, utalii na mchango wa sekta hizo katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kiasi cha **TZS 2,23.541 bilioni** kimetumika kwa ajili ya Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo.

### q.Maendeleo ya Teknolojia na Mawasiliano

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuimarisha juhudi za kukuza ajira, kuendeleza vipaji, na kuweka mazingira wezeshi yanayochochea ubunifu na ushiriki mpana wa wananchi katika shughuli za kiuchumi. Hali hii imechochewa kwa kasi zaidi mara tu baada ya kukamilika kwa uchaguzi mkuu, kupitia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kuunda Wizara maalum inayosimamia masuala ya Mawasiliano, Teknolojia na Ubunifu.

**115.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Tathmini, Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

- i Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na kukuza mazingira ya ubunifu na teknolojia nchini;
- ii Kuongeza matumizi ya mifumo katika utoaji wa huduma za Serikali kwa ufanisi zaidi katika sekta zote za maendeleo;

iii Kuwekeza katika Mfumo wa Mkonga wa Taifa na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika Miundo mbinu ya kidijitali. Jumla ya vituo 153 kati ya 211 vimepelekewa mkonga wa kitaifa wa mawasiliano (Unguja 101 na Pemba 52);

iv Kutunga sera ya Kidijitali Zanzibar ya Mwaka 2026, kufuatia mapitio ya sera ya TEHAMA ya Zanzibar ya Mwaka 2013; na

v Kukamilisha rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa binafsi ya Mwaka 2026 (the Personal Data Protection Act,2026).

**r. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**116. Mheshimiwa Spika,** Maendeleo yoyote yanahitaji ushirikishwaji mpana wa wananchi katika shughuli za kiuchumi kupitia uwekezaji katika ujuzi, mitaji na fursa za uzalishaji. Katika kufanikisha hilo, juhudi zinaelekezwa katika kujenga mazingira wezeshi yatakayoongeza ajira, kuinua kipato cha wananchi na kuimarisha ustawi wa jamii kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Kwa kipindi cha tathmini kiasi cha **TZS 7.455 bilioni** zimetumika kwa ajili ya mradi wa Ujenzi wa vituo vya Maendeleo ya Vijana na Mradi wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa.

**117. Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi, **TZS 12.779 bilioni** zilitolewa na Serikali kama mikopo kwa wananchi **6,135** kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Aidha, **TZS 5.668** bilioni zimekusanywa kama marejesho ya mikopo.

118. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imechukua hatua kadhaa kwa lengo la kujenga matumaini mapya na kuhakikisha kuwa maendeleo yanakuwa jumuishi na kwa manufaa ya wote zikiwemo:

i Kuanza utoaji wa mikopo binafsi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi;

ii Kuandaa moduli za mafunzo ya ujasiriamali kwa lengo la kusaidia utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali;

iii Kuanzishwa kwa programu ya Mfuko wa Dkt. Mwinyi Boosting Fund, ambapo jumla ya wanawake wajasiriamali wadogo 4,021 wamenufaika; na

iv Wajasiriamali 101 (wanaume 30 na wanawake 71) na Kampuni 50 za Wajasiriamali wameunganishwa na fursa za masoko kwa kupitia maonesho mbali mbali.

### s.Ukamilishaji na Uendelezaji wa Miradi ya Kimkakati

119. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza kwa ufanisi miradi mbalimbali ya maendeleo inayolenga kuimarisha huduma za kijamii na kukuza shughuli za kiuchumi. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali imeendelea kuelekeza rasilimali fedha kwa ajili ya Kuendeleza na Kukamilisha Miradi ya Maendeleo ya Kipaumbele ili kuhakikisha uwekezaji uliokwisha kufanyika unazalisha matokeo yaliyokusudiwa na kuwanufaisha wananchi kwa wakati. Katika kipindi cha miezi tisa cha tathmini ya utekelezaji wa Bajeti, tumeshuhudia Miradi kadhaa ikiendelezwa ujenzi ikiwemo:

- Ujenzi wa Daraja la Uzi Ng'ambwa (6.5km);
- Ujenzi wa Barabara za juu "Flyover";
- Ujenzi wa Chuo kikuu cha Suza Main Campus Tunguu;
- Ujenzi wa Vituo vya Afya;
- Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi;
- Ujenzi wa Bandari ya uvuvi Shumba;
- Ujenzi wa Nyumba za Chumbuni;
- Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa;
- Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa;
- Mradi wa Kituo cha mabasi ya Umeme malindi; na
- Hospitali ya wagonjwa wa Afya ya Akili Pandani.

120. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo, ili kuhakikisha inakamilika kwa viwango vinavyotakiwa, ndani ya muda uliopangwa na kwa gharama stahiki. Hatua hii itasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi nchini.

121. **Mheshimiwa Spika,** Tumekuwa tukiwaona viongozi wetu wakuu wa Serikali, Mawaziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Viongozi wa taasisi mbalimbali wakifanya ziara za mara kwa mara na tathmini ya Maendeleo ya Miradi inayotekelezwa nchini. Ziara hizo zimekuwa nyenzo muhimu katika kutathmini mwenendo wa utekelezaji wa miradi, kubaini changamoto zinazojitokeza kwa wakati, kuharakisha utoaji wa maamuzi ya kiutendaji na kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa

ufanisi, tija na kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money). Hatua hiyo imechangia kuimarika kwa kasi ya utekelezaji wa miradi, kuongezeka kwa uwajibikaji wa wakandarasi na wasimamizi wa miradi, pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanaanza kunufaika na matokeo ya uwekezaji wa Serikali kwa wakati uliokusudiwa.

## H. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI-JUNI KWA MWAKA 2025/2026

### H.1 MAPATO

122. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, hadi kukamilika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mwezi wa Juni 2026, Serikali inatarajia kukusanya **TZS 6,386.88 bilioni** sawa na asilimia 91 ya makadirio ya **TZS 6,982.076 bilioni.**

### H.1.1 Mapato ya Ndani

123. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia **TZS 2,687.75 bilioni** sawa na asilimia **97.5** ya makadirio ya mwaka yanayojumuisha:-

#### a. Mapato ya kodi

124. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia **TZS 2,051.39 bilioni**, sawa na asilimia 97.5 ya makadirio ya TZS 2,104.01 bilioni, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania-Zanzibar (TRA) inatarajiwa kukusanya TZS 825.08 bilioni sawa na asilimia 99.9 ya makadirio;

ii. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatarajiwa kukusanya TZS 1,205.32 bilioni sawa na asilimia 96; na

iii. Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT inatarajiwa kufikia TZS 21 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

**b. Mapato yasiyokuwa ya kodi**

**125. Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 275.95 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio ya TZS 293.82 bilioni kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mapato ya Wizara yanategemewa kufikia TZS 242.45 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio;

ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 20 bilioni sawa na asilimia 80 ya makadirio; na

iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 13.5 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio.

**c. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

**126. Mheshimiwa Spika,** Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia **TZS 919.14 bilioni** sawa na asilimia 64 ya makadirio ya TZS 1,444.842 bilioni, kwa mchanganuo ufuatao:

i. Misaada ya Kibajeti (General Budget Support) inatarajiwa kufikia TZS 120 bilioni, sawa na asilimia 100 ya makadirio;

ii. Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo (Basket Fund) unatarajiwa kufikia TZS 0.50 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio;
iii. Misaada kutoka Washirika kwa Maendeleo inatarajiwa kufikia TZS 225.91 bilioni sawa na asilimia 62 ya makadirio; na
iv. Mikopo nafuu ya kisekta inatarajiwa kufikia TZS 572.72 bilioni, sawa na asilimia 59 ya makadirio.

### H.1.2 Mkopo wa Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

127. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio ni kupokea TZS 2,780.00 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio kati ya Mkopo huo:

i. TZS 1,080.00 bilioni Mkopo wa Hati Fungani; na
ii. Mkopo kutoka Taasisi za kifedha na benki kwa kugharamia Miradi ya Maendeleo TZS 1,700.00 bilioni.

### H.1.3 Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zinazojitegemea (Own sources)

128. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa matarajio ni kukusanya TZS 19.2 bilioni sawa na asilimia 89 ya makadirio na Taasisi zinazojitegemea matarajio ni kukusanya TZS 341.2 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio.

## H.2 MATUMIZI

129. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kufikia Juni 2026, yanatarajiwa kufikia **TZS 6,354.58 bilioni** sawa na asilimia 91 ya bajeti ya mwaka ya **TZS 6,982.076 bilioni** kwa mchanganuo ufuatao:

   i. Matumizi kwa Kazi za Kawaida yanatarajiwa kufikia **TZS 2,293.37 bilioni** (zikiwemo TZS 12.4 bilioni za Mamlaka za Serikali za Mitaa na TZS 341.20 bilioni kwa Taasisi zinazojitegemea);

   ii. Matumizi kwa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo matarajio ni kutumia **TZS 4,054.41 bilioni** sawa na asilimia 89 ya makadirio; na

   iii. TZS 6.8 bilioni kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

130. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali inatarajia kuwa na bakaa ya **TZS 32.3 bilioni** kwa ajili ya matumizi ya awali ya mwaka mpya wa fedha 2026/27. **Kiambatisho Nambari 4**: Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi kufikia Juni 2026.

131. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Juni 2026, Serikali inatarajia kupokea Mkopo wa kiasi cha **TZS 1,890.0 bilioni** kwa ajili ya kuziba nakisi ya bajeti, ambapo kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu na makubaliano na Benki mbalimbali ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya kupata mkopo huo.

## I. MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026

132. **Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar mwaka 2026 unatarajiwa kuimarika zaidi, sekta zinazotarajiwa kukua kwa kasi kubwa zaidi ni pamoja na sekta ya miundombinu, biashara, uwekezaji, sekta za huduma na viwanda.

### I.1 MALENGO NA SHABAHA ZA UCHUMI JUMUISHI KWA MWAKA 2026

133. **Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2026, kwa takwimu za awali ni kukua kwa **asilimia 7.5** Mwaka 2026 kutoka ukuaji wa **asilimia 7.0** Mwaka 2025 kutokana na sababu ambazo tayari tumeshaziwasilisha kupitia Hotuba iliyowasilishwa asubuhi hii, zikiwemo:

i Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 9.3 kutoka watalii 917,167 kwa mwaka 2025 hadi watalii 1,002,917 mwaka 2026;

ii Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa Mji wa Serikali, Ujenzi wa bandari ya Mangapwani na Mpigaduri na Ujenzi wa Mji wa Michezo (AFCON City) Fumba; na

iii Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu na kuimarisha Matumizi endelevu ya Bahari.

**134. Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo yanategemea na misingi ifuatayo:

i Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;

ii Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;

iii Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;

iv Kuwa na uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa kwa matumizi ya ndani na usafirishaji nje ya nchi;

v Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha timu kwa mazoezi na baadhi ya mechi za Mashindano ya kuwania Kombe la Afrika (AFCON); na

vi Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani.

**135. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo:

i Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;

ii Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;

iii Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani;

iv Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;

v Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na

vi Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku hasa kwa vyakula vikuu vinavyolimwa hapa nchini.

## J.MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

136. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kuweka mfumo wa kodi uliotulivu na wenye kutabirika, kushajihisha ulipaji wa kodi kwa hiari, kukuza ajira, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi katika Sekta mbali mbali nchini. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato.

137. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni kama zifuatavyo:

### A.Hatua Zinazohusu Marekebisho ya Sheria

### Kuongeza Wigo wa Ukusanyaji wa Mapato

### J.1 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017

i. **Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye Viwanja vya Michezo, Kumbi za Starehe na Maeneo ya Burudani (Luxuries Goods & Services)**

138. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa nyenzo "**fiscal instrument"** zinazotumiwa na Serikali nyingi duniani ni kutoza kodi kwa uingizaji au usambazaji wa bidhaa na huduma za kifahari (Luxuries Goods & Services) ili kuleta usawa katika mfumo wa kodi. Hivyo, Serikali inapendekeza kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia kumi (10%) kwenye tiketi za kiingilio katika Viwanja vya Michezo, Kumbi za Starehe na Maeneo ya Burudani. Aidha, inapendekezwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuweka mifumo ya kielektroniki kwa ajili ukataji wa tiketi katika viwanja vya michezo. Hatua hii inatarajiwa kukusanya **TZS 2.27 bilioni** ambapo, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya uimarishaji wa viwanja vya michezo nchini.

ii. **Kuoanisha Kiwango cha Utozaji wa Ushuru wa Bidhaa kwa Usambazaji wa Huduma za Kampuni Zinazorusha Matangazo ya Televisheni (Cable Television Company)**

139. **Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imekuwa ikitoza ushuru wa bidhaa kwa kampuni zinazorusha matangazo ya Televisheni kwa kiwango cha asilimia tano (5%) wakati Tanzania Bara hutoza huduma kama hizo kwa kiwango cha asilimia saba (7%). Hali hii imepelekea kupotea kwa mapato ya Serikali kwani kifurushi cha mwezi kinauzwa bei sawa kati Zanzibar na Tanzania Bara bila ya kujali kiwango kidogo cha ushuru

wa bidhaa kinachotozwa Zanzibar. Hivyo, inapendekezwa kuoanisha kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa kampuni zinazorusha matangazo ya Televisheni (Cable Television Company) kuwa Asilimia saba (7%). Hatua hii inatarajiwa kukusanya **TZS 1.27 bilioni**.

iii. **Kuwaingiza katika Wigo wa Kodi Wasambazaji Wasio Wakaazi (non-resident) Wanaotoa Huduma za "Live streaming and advertising" Zinazotozwa Ushuru wa Bidhaa**

140. **Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu mfumo wetu wa kodi ulikuwa ikitoza ushuru wa bidhaa kwa huduma za "Live streaming and advertising" zinazotolewa na wasambazaji wakaazi bila ya kuwatoza ushuru huo wasambazaji wasio wakaazi (non-resident). Hali hii hupunguza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao 2026/27, inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa huduma zinazotolewa na wasambazaji wasio wakaazi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.72 bilioni.**

iv. **Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Kiwango cha 5% kwa Uingizaji wa Gari zenye Uwezo wa Ingini chini ya 1,000 CC**

141. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 5% kwa uingizaji wa gari zenye uwezo wa ingini chini

ya 1,000CC ili kuleta usawa katika mfumo wa kodi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.75 bilioni.**

## J.2 Marekebisho ya Sheria ya Biashara Zanzibar Namba 14 ya Mwaka 2013

### i. Kuongeza Kiwango cha Tozo ya Uingizaji wa Vyombo vya Moto (Motor Vehicle Levy)

**142. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha ujao 2026/27, Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kama ifuatavyo:

a. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa uingizaji wa pikipiki kutoka TZS 30,000 hadi TZS 50,000;

b. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa uingizaji wa gari kutoka TZS 100,000 hadi TZS 200,000;

c. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa usafirishaji wa gari kutoka Zanzibar kutoka TZS 20,000 hadi TZS 50,000;

d. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa usafirishaji wa pikipiki kutoka TZS 15,000 hadi TZS 30,000;

e. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa usafirishaji wa “truck” au “trailer” kutoka TZS 10,000 hadi TZS 20,000; na

f. Kutoza tozo ya uingizaji wa vyombo vya moto (motor vehicle levy) kwa usafirishaji wa gari kutoka Tanzania Bara kutoka TZS 100,000 hadi TZS 200,000.

**143. Mheshimiwa Spika,** Hatua hizi zinatarajiwa kukusanya **TZS 2.25 bilioni**.

### J.3 Marekebisho ya Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari Namba 2 ya Mwaka 1999

#### i. Kuongeza Kiwango cha Ada ya Huduma za Bandari kwa Wageni Wanaosafiri Ndani ya Zanzibar (Pemba/Unguja) au Zanzibar kwenda Tanzania Bara

**144. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 Serikali inapendekeza kuongeza ada ya huduma za bandari kwa wageni (non-residents) wanaosafiri ndani Zanzibar (Pemba/ Unguja) na kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kutokana na viwango hivyo kupitwa na wakati na kutoendana na hali halisi ya Uchumi wa Zanzibar, kama ifuatavyo:

a. kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kutoka $ 2 hadi $ 3; na
b. kutoka Unguja kwenda Pemba kutoka $ 1 hadi $ 2.

**145. Mhshimiwa Spika,** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali **TZS 1.75 bilioni**.

**J.4 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

i. **Kuongeza Kiwango cha Kodi ya Miundombinu kwa Wageni Wanaosafiri Ndani ya Zanzibar (Pemba/Unguja) au Zanzibar kwenda Tanzania Bara**

146. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitoza Kodi ya Miundombinu kwa wageni (non-residents) wanaosafiri ndani ya Zanzibar (Pemba/Unguja) kwa USD 1 na Zanzibar kwenda Tanzania Bara kwa USD 2. Aidha, viwango hivyo vimepitwa na wakati pamoja na kutoendana na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar. Hivyo, inapendekezwa kuongeza kiwango cha kodi ya miundombinu kama ifuatavyo:

a. USD 3 kwa wageni wanaosafiri kwenda Tanzania Bara; na

b. USD 2 kwa wageni wanaosafiri ndani ya Zanzibar.

147. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali **TZS 1.75 bilioni**.

**Kuimarisha Udhibiti na Usimamizi wa Forodha**

**J.5 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Namba 8 ya Mwaka 2017**

i. **Kuanza kutoza Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kwa Uingizaji wa Soseji na Bidhaa Nyengine zinazofanana na hizo**

148. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 inapendekezwa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha TZS 500 kwa kilo kwa uingizaji wa Soseji na bidhaa nyengine

zinazofanana na hizo ili kudhibiti matumizi ya bidhaa hizo nchini.

ii. **Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Kiwango cha 20% kwa Uingizaji wa Mashine za Kukausha Kucha kwa Kutumia Mionzi ya "Ultra Violet/Led"**

**149. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya mashine za kukausha kucha hutoa mionzi ya "Ultra Violet/Led", ambayo husababisha madhara na kuongeza hatari ya saratani. Hivyo, inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 20% ili kudhibiti matumizi ya mashine hizo.

iii. **Kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa Kiwango cha 20% kwa Uingizaji wa "Maua, Majani na Matunda Bandia (Artificial Flowers, Foliage & Fruits)**

**150. Mheshimiwa Spika,** Uingizaji wa maua, majani na matunda bandia yaliyotengenezwa kwa vifaa visivyoharibika kiasili (non-biodegradable materials) huchangia katika uharibifu wa mazingira pamoja na kuongeza changamoto za usimamizi wa taka nchini. Hivyo, ili kupunguza pamoja na kudhibiti uharibifu wa mazingira nchini, inapendekezwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha 20% kwa uingizaji wa Maua, Majani na Matunda Bandia (Artificial Flowers, Foliage & Fruits).

**iv. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Vipodozi kutoka 10% to 15%**

151. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27 inapendekezwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka 10% hadi 15% ili kudhibiti matumizi ya bidhaa hizo nchini.

**v. Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa Wigi, Nywele bandia, kope za bandia, kucha za bandia na bidhaa nyengine zinazofanana na hizo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kunmekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya Wigi, Nywele bandia, kope za bandia, kucha za bandia na bidhaa nyengine zinazofanana na hizo. Hivyo, inapendekezwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kutoka 25% hadi 30% ili kudhibiti matumizi ya bidhaa hizo nchini ambazo ni hatari kwa afya ya binadamu. Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.37 bilioni.**

**vi. Kuongeza Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwa Uingizaji wa Mvinyo, Vinywaji Vikali, Bia na Sigara**

152. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa mvunyo, vinywaji vikali na Bia kama ifuatavyo: -

i. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa vinywaji vikali (spirit) kutoka TZS 6,000 hadi TZS 7,000 kwa lita;

ii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa mvinyo (wine) kutoka TZS 6,000 hadi TZS 7,000 kwa lita;

iii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa Bia kutoka TZS 803 hadi TZS 1,500 kwa lita; na

iv. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa uingizaji wa Sigara kutoka TZS 55,896 hadi TZS 65,000 kwa mil.

Hatua hizo zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 1.25 bilioni**, ambapo fedha zake zitatumika kwa ajili ya kuimarisha huduma za Afya nchini.

**Kuimarisha Miundombinu ya Usafirishaji wa Anga**

**J.6 Marekebisho ya Sheria ya Fedha Namba 9 ya Mwaka 2015**

**i. Kuongeza Kiwango cha Kodi ya Miundombinu kwa Abiria Wanaosafiri kwa Ndege**

**153. Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa, Serikali imekuwa ikitoza Kodi ya Miundombinu kwa abiria wanaosafiri kwa ndege kwa kiwango cha TZS 2,000. Aidha, kiwango hicho kimepitwa na wakati na hakiendani na hali halisi ya uchumi wa Zanzibar. Hivyo, inapendekezwa kuongeza kiwango cha kutoza Kodi ya Miundombinu kwa abiria wanaosafiri kwa ndege kutoka TZS 2,000 hadi TZS 4,000 ili kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa anga nchini. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato kwa **TZS 0.75 bilioni**.

**Kurahisisha Upatikaji wa Vifaa Vinavyotumiwa na Watu Wenye Mahitaji Maalum**

i. **Kutoa Unafuu wa Kodi ya Miundombinu kwa Uingizaji wa Vifaa Vinavyotumiwa na Watu Wenye Ulemavu Maalum**

154. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kwamba, watu wenye mahitaji maalum wanapata vifaa saidizi kwa gharama nafuu, inapendekeza kutoa unafuu wa Kodi ya Miundombinu kwa uingizaji wa Viti Mwendo (wheel chairs), viungo bandia (Artificial Limbs and Hands), visaidizi vya kuona na kusomea (programmable hearing aids), Fimbo Nyeupe (white canes) na Mashine za Kutolea Hati Nundu (Brailler Machine) na vyoo vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu (toilet for disabled person).

**Kushajihisha Ulipaji wa Kodi kwa Hiari**

**J.7 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya Mwaka 2017**

i. **Kupunguza Kiwango cha Ushuru wa Stempu kwa 25% kwa Magari ya Biashara Pamoja na Kuweka Utaratibu wa Malipo Ushuru huo Wakati wa Upasishaji wa Gari**

155. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa changamoto kutoka kwa walipakodi wa gari za biashara kushindwa kulipa kodi kwa hiari kutoka na viwango vikubwa vya kodi. Hali hii hupunguza ari ya uliaji wa kodi kwa hiari pamoja na kuongeza gharama za usimamizi wa kodi. Hivyo, inapendekezwa kupunguza

kiwango cha ushuru wa stempu kwa 25% kwa magari ya biashara, pamoja na kuweka utaratibu wa malipo ya ushuru huo wakati wa upasishaji wa gari. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.79 bilioni**.

**Kuimarisha Uzalishaji katika Sekta Binafsi**

**J.8 Marekebisho ya Sheria ya Mafunzo ya Amali, Namba 8 ya Mwaka 2006**

**i.Kupunguza Kiwango cha Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL)**

**156. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, Serikali inapendekeza kupunguza kiwango cha Tozo ya Kuendeleza Ujuzi (SDL) kutoka asilimia nne (4%) hadi asilimia tatu (3%) ili kukuza ujuzi kwa vijana na kuweza kujiajiri. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa **TZS 3.7 bilioni**.

**J.9 Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya Mwaka 1998**

**i.Kutoa Unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Uingizaji wa "Boarding Passes" na "Airlines Ticket"**

**157. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kwamba, Serikali inakwenda sambasamba na miongozo ya kimataifa duniani katika Sekta ya Anga ikiwemo "International Civil Aviation Organization (ICAO)", inapendekezwa kutoa unafuu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa uingizaji wa "boarding passes" na "airlines tickets".

## J.10 Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya Mwaka 2017

### i. Kutoa Unafuu wa Ushuru wa Stempu kwa Ununuzi wa Tiketi za Ndege kwa Mashirika ya Ndege ya Ndani "Domestic Airliner"

**158. Mheshimiwa Spika,** ununuzi wa tiketi za ndege kwa mashirika ya ndege ya ndani hutozwa ushuru wa stempu kwa kiwango cha 3% kwa tiketi, wakati ununuzi wa tiketi za ndege kwa mashirika ya kimataifa hayatozwi ushuru wa stempu. Hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao 2026/27 inapendekezwa kutoa unafuu wa ushuru wa stempu kwa ununuzi wa tiketi za ndege kwa mashirika ya ndege ya ndani ili kuendana na miongozo ya kimataifa "International Civil Aviation Organization (ICAO)" pamoja na kupunguza gharama za ununuzi wa tiketi kwa wananchi. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa **TZS 0.7 bilioni**.

## Kuimarisha Uwekezaji katika Viwanda Vidogo na Kati

### i. Kutoa Unafuu wa Kodi kwa Uingizaji wa Malighafi kwa Viwanda Vidogo na Kati

**159. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha na kuchochea uwekezaji wa viwanda vidogo na kati nchini. Serikali inapendekeza kutoa unafuu wa kodi kwa wawekezaji wa viwanda Vidogo na Kati ambao hawajasajiliwa katika Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kwa uingizaji

wa malighafi nchini. Hatua hiyo inatarajiwa kushajihisha wawekezaji katika sekta ya uzalishaji nchini pamoja na kuimarisha uchumi.

**B.Hatua za Kuimarisiha Utawala na Usimamizi wa Kodi**

**i. Kudhibiti Matumizi Mabaya ya Misamaha ya Kodi**

**160. Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na matumizi mabaya ya misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali kwa baadhi ya miradi ya wawekezaji, miradi inayofadhiliwa na Serikali, na miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo. Hali hii hupelekea kupunguza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hivyo, ili kuondokana na changamoto hizo, Serikali itaunda timu ya wataalamu itakayojumuisha wajumbe kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka yaa Mapato Zanzibar (TRA na ZRA) kwa ajili ya kusimamia ufuatiliaji wa matumizi mabaya ya misamaha iliyotolewa na Serikali. Aidha, iwapo bidhaa (vifaa) zilizopewa msamaha zitatumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa au kuhamishwa, kuuzwa au kutolewa kwa njia yoyote kwa mtu mwengine ambae hana haki ya kupata msamaha huo, hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria.

**161. Mheshimiwa Spika,** Serikali inasisitiza kuwa; Wizara, Taasisi na Idara zinazojitegemea wakati wanapoingia mkataba na Mtu Binafsi, Mkandarasi au Mshauri Elekezi, ambao una kipengele cha msamaha wa kodi, tozo au ada kuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwa ajili ya kupata ridhaa yake kabla mkataba husika kusainiwa. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali itakuwa na jukumu la kuthibitisha kuwa mkataba wenye kipengele cha msamaha wa kodi, tozo au ada umepata ridhaa ya Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

162. **Mheshimiwa Spika,** Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **TZS 5.72 bilioni**.

**ii. Kuweka Kituo Kimoja cha Huduma kwa Walipakodi (One - Stop Tax Centre)**

163. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na changamoto kwa walipakodi waliosajiliwa na TRA & ZRA kufuata huduma za walipakodi kwa mamlaka mbili tofauti za kodi (TRA&ZRA). Hali hii inapoteza muda na kuleta usumbufu kwa walipakodi. Hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao 2026/2027 inapendekezwa kuweka kituo kimoja cha huduma kwa walipakodi (One - Stop Tax Centre) kitakachotoa huduma za kodi zinazosimamiwa na TRA na ZRA ili kurahisisha upatikanaji wa huduma pamoja na kupunguza usumbufu kwa walipakodi.

**iii. Kufanya Ukaguzi na Uchunguzi wa Kodi wa pamoja Kati Mamlaka za Usimamizi wa Kodi (TRA na ZRA)**

164. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya walipakodi waliosajiliwa na TRA na ZRA, ambapo kila taasisi hufanya ukaguzi na uchunguzi wa kodi kwa wakati wake. Hali hii inapelekea usumbufu kwa walipakodi, kuongeza gharama za ulipaji wa kodi kwa walipakodi

pamoja na gharama za usimamizi wa kodi kwa Mamlaka za Usimamizi wa Kodi TRA na ZRA. Hivyo, kwa mwaka wa fedha ujao 2026/2027 Serikali inapendekeza kufanya ukaguzi na uchunguzi wa kodi wa pamoja kati ya Mamlaka za Usimamizi wa Kodi TRA na ZRA ili kupunguza gharama na usumbufu kwa walipakodi pamoja na gharama za usimamizi wa kodi.

## K. MKAKATI WA SERIKALI KWA MWAKA 2026/2027

165. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2026/2027, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuimarisha uchumi, kuongeza uzalishaji, kuboresha utoaji wa huduma za jamii na kuimarisha ustawi wa wananchi. Aidha, Serikali itaendelea kuweka mkazo katika usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma, uwekezaji katika miundombinu pamoja na kuendeleza mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Maeneo yafuatayo yataendelea kupewa kipaumbele.

### a. Kuharakisha Upatikanaji wa Nishati ya Umeme wa uhakika, endelevu na gharama nafuu

166. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua umuhimu wa nishati ya umeme katika kuchochea ukuaji wa uchumi, uwekezaji na ustawi wa wananchi, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Serikali itaelekeza juhudi zaidi katika kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, kuongeza matumizi ya nishati jadidifu, pamoja na kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme unaokidhi mahitaji ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Taifa.

## b. Kuimarisha Mawasiliano, Teknolojia na Ubunifu

167. **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu dunia inaelekea kwenye matumizi makubwa ya akili bandia (AI), biashara mtandao na mifumo ya kisasa ya mawasiliano ili kukabiliana na mahitaji ya sasa ya kidijitali na kukuza ubunifu wa vijana, kuongeza ufanisi wa huduma za Serikali na kuimarisha ushindani wa uchumi wa Zanzibar katika mazingira ya uchumi wa dunia yanayobadilika kwa kasi.

168. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kuchukua hatua mahsusi za kimkakati ili kuendana na dhamira ya kuharakisha mapinduzi ya kidijitali ikiwemo, kuwepo na Sera ya Kidijitali ya Zanzibar ya Mwaka 2026 (Zanzibar Digital Policy, 2026) ambayo ni hatua muhimu ya kimkakati inayolenga kuharakisha mabadiliko hayo. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kiasi cha **TZS 41.365 bilioni** zimetengwa kwa ajili ya Programu ya mageuzi ya kidigitali ambayo imelenga kuanzisha Mji wa Teknolojia na Mfumo wa Serikali wa kubadilishana taarifa.

## c.Kuimarisha Mapato ya Ndani

169. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha mapato ya ndani yanakusanywa kwa ufanisi mkubwa. Miongoni mwa Mikakati hiyo ni pamoja na:

i. Kuunganisha mifumo ya biashara na mifumo ya ukusanyaji kodi (Digital Transformation & Systems Integration) ikiwemo:

- Mfumo wa VFMS kwa walipakodi ambao wanatumia mifumo binafsi kuendesha biashara zao, wakiwemo; Biashara za Mahoteli, Watembeza Wageni, Mifumo ya Kufanya Malipo "Pesapal", MasterCard, na VISA;
- Kusajili wafanyabiashara wa kimataifa katika maeneo ya utalii na biashara mtandao;

ii. Kuimarisha Usajili na Upanuzi wa Wigo wa Kodi kwa kufanya operesheni za usajili kwa sekta zisizo rasmi na kuanzisha utaratibu wa "Formalization First" kwa biashara za utalii;

iii. Kuimarisha Ukaguzi na Uchunguzi wa Kodi kwa Kuongeza Tax Audits kwa Walipakodi wakubwa, wa kati na Desk Audits kwa walipakodi wadogo sambamba na Kuimarisha kazi za Idara ya Uchunguzi wa Kodi ili kudhibiti ukwepaji kodi;

iv. Kusimamia viashiria hatarishi kwenye uwajibikaji wa kulipa kodi (Compliance Risk Management); na

v. Kupunguza mianya ya ukwepaji wa kodi na upotevu wa mapato kwa kuimarisha matumizi ya teknolojia, uchambuzi wa takwimu, na ushirikiano kati ya taasisi za ukusanyaji wa mapato.

### d.Matumizi ya Takwimu katika Kuimarisha Uchumi

**170. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, Serikali itaendelea kuweka mkakati wa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, uzalishaji, usambazaji na matumizi ya

takwimu rasmi, kupitia mfumo jumuishi wa ukusanyaji wa taarifa za kitakwimu katika Wizara na Taasisi za Serikali.

171. **Mheshimiwa Spika,** Mkazo utaendelea kuwekwa katika maeneo yafuatayo:

i. Kuimarisha uwekezaji katika teknolojia za kidijitali, na mifumo ya taarifa ili kuhakikisha upatikanaji wa takwimu kwa wakati, usahihi na uwazi zaidi. kupitia mfumo wa Zanzibar Statistical Information System" (ZANSIS) na mfumo wa Tanzania Intergrated Statistical Portal (TISP);
ii. Kutathmini na kutekeleza Sera na Mipango ya Maendeleo ya Taifa kwa matumizi ya takwimu sahihi na za kuaminika kama msingi wa ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu;
iii. Kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi, uwazi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya wananchi;
iv. Kutathmini athari za sera za kiuchumi, kuongeza uzalishaji takwimu za msingi zitakazosaidia na kuboresha upangaji wa bajeti inayozingatia matokeo (Program Based Budgeting-PBB);
v. Kuimarisha matumizi ya Sayansi ya Data, akili bandia pamoja na ubunifu wa kitakwimu, na
vi. Kufanya uchambuzi wa matumizi ya takwimu kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa, ili kuhakikisha kuwa maamuzi yote ya kiuchumi yanategemea ushahidi (evidence-based decision making).

### e. Usimamizi na Ufanisi Matumizi ya Fedha za Umma

172. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa lengo la kuhakikisha thamani halisi ya fedha (value for money) katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wananchi unazidi kuimarika.

173. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya nane imekuwa ikisimamia nidhamu na matumizi ya fedha kwa vitendo, sisi kama viongozi ambao tumepewa dhamana ya usimamizi wa fedha hatukuwa tu jukumu letu la kusimamia na kuzigawanya kwa sekta, badala yake tunahakikisha fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa malengo sambamba na kufuatilia matumizi ya fedha hizo katika maeneo yote ya miradi ya kimkakati na kushuhudia matumizi halisi ya fedha hizo. Miongoni mwa maeneo ambayo yamewekewa mkazo zaidi ni pamoja na:

i. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini (Monitoring and Evaluation), pamoja na kuhakikisha kuwa kila shilingi inayotumika inaleta matokeo yanayokusudiwa;

ii. Kuhakikisha rasilimali zinapelekwa kwenye maeneo yenye tija kiuchumi na kijamii, kudhibiti upotevu wa rasilimali na kuimarisha nidhamu ya matumizi katika taasisi zote za umma;

iii. Kuimarisha matumizi ya viashiria vya utekelezaji (performance indicators) ili kupima ufanisi wa matumizi ya bajeti, kwa kuangalia uwiano kati ya rasilimali

zilizotengwa na matokeo yanayopatikana (input-output linkage);

iv. Kukamilisha uandaaji wa sera ya ununuzi wa umma. ambayo itaimarisha mfumo wa ununuzi wa umma na kuleta mabadiliko ya udhibiti rasilimali fedha na Usimamizi wa mikataba kwa ufanisi sambamba na kusimamia watumishi wa kada juu ya uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za manunuzi ya umma, na kuongeza matumizi ya mifumo ya kidijitali katika usimamizi wa manunuzi ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika mchakato mzima wa ununuzi; na

v. Kupunguza uhamishaji wa mafungu ya bajeti baina ya Taasisi (Virement) na Uhaulishaji wa vifungu ndani ya Taasisi (Realocation).

## L.MAPENDEKEZO YA SURA YA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**174. Mheshimiwa Spika,** Katika mazingira ya uchumi wa dunia yanayoendelea kubadilika kwa kasi kutokana na changamoto za kiusalama, mabadiliko ya teknolojia, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa. Ushirikiano wa kikanda umeendelea kuwa nguzo muhimu ya kuimarisha ustahamilivu wa uchumi na ustawi wa wananchi. Kwa kutambua umuhimu huo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kuimarisha juhudi za pamoja za kukuza biashara, uwekezaji, usalama na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wa ukanda huu.

**175. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeweka msisitizo katika kuimarisha usalama wa kikanda, kuongeza uwezo wa nchi wanachama wa kuhamasisha na kusimamia mapato ya ndani, pamoja na kuharakisha matumizi ya teknolojia za kidijitali kama nyenzo muhimu za kuchochea ukuaji wa uchumi unaojumuisha makundi yote ya jamii. Mwelekeo huu unalenga kujenga uchumi wenye uwezo wa kukabiliana na mishtuko ya ndani na nje, kuongeza ushindani wa kanda katika soko la kimataifa na kuimarisha fursa za ajira, biashara na uwekezaji.

**176. Mheshimiwa Spika,** Kwa muktadha huo kaulimbiu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni: **"Kuimarisha Ustahamilivu wa Uchumi wa Zanzibar kupitia Kuongeza Mapato ya Ndani, Kuharakisha Mageuzi ya Kidijitali na Kukuza Ushirikiano wa Kikanda kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu.** yaani *"Strengthening Zanzibar's Economic Resilience through Enhanced Domestic Revenue Mobilization, Digital Transformation, and Regional Integration for Inclusive and Sustainable Growth."* kaulimbiu hii imetokana na Kauli Mbiu ya pamoja ***"Deepening Regional Intergration and Economic Resilience through improved Regional Security, Domestic Revenue mobilisation and Digital Transformation for inclusive Growth".***

**177. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kaulimbiu hii inaendana kikamilifu na azma ya kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kuongeza

mapato ya ndani, kuendeleza uchumi wa kidijitali, kuvutia uwekezaji na kuimarisha ushiriki wa Zanzibar katika fursa zinazotokana na ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Kupitia jitihada hizi, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayochochea ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kuboresha ustawi wa wananchi kwa ujumla.

**178. Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Mapato ambayo tunayawasilisha leo kuomba idhini ya Baraza lako tukufu, yamezingatia uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kulingana na vigezo na shabaha za kiuchumi na maoteo (projections) kutokana na ahadi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Mikakati ya Kitaifa.

### L.1 Mwelekeo wa Ukusanyaji wa Mapato

**179. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2026/2027, mapato ya Serikali yanakadiriwa kufikia **TZS 8,525.850 bilioni** ikiwa ni ongezeko la TZS 1,543.773 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 22.11 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2025/2026 ya **TZS 6,982.076 bilioni**. Makadirio hayo yanatokana na mageuzi ya sera na mikakati mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato sambamba na mikopo nafuu ya ndani ambayo Serikali inapanga kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Kimkakati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

#### L.1.1 Mapato ya ndani

**180. Mheshimiwa Spika,** Mapato ya ndani yanajumuisha Mapato ya Kodi na Yasiyokuwa ya Kodi, Mikopo ya Ndani

na Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mapato ya Taasisi Zinazojitegemea.

181. **Mheshimiwa Spika,** Mapato hayo yanakadiriwa kufikia **TZS 7,011.454 bilioni** ikiwa ni ongezeko la **TZS 1,474.219 bilioni** sawa na ukuaji wa asilimia 26.62 ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka 2025/2026 ya **TZS 5,537.235 bilioni,** kwa mchanganuo ufuatao:

i. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) **TZS 1,726.661 bilioni**;

ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) upande wa Zanzibar **TZS 1,144.690 bilioni**;

iii. Mapato ya kodi za wafanyakazi kutoka SMT (PAYE) walioko Zanzibar **TZS 21 bilioni;**

iv. Mapato yasiyokuwa ya kodi **TZS 356.796 bilioni**;

v. Mikopo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni **TZS 3,400.000 bilioni**;

vi. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa **TZS 25.996 bilioni;** na

vii. Mapato ya Taasisi zinazojitegemea za Serikali **TZS 336.311 bilioni**.

### L.1.2. Mapato yatokanayo na Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

182. **Mheshimiwa Spika,** Mapato yatokanayo na misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanakadiriwa kufikia **TZS 1,514.396 bilioni;** ikiwemo (mikopo ya TZS 1,105.251 bilioni na misaada TZS 258.613 bilioni, TZS 0.532 bilioni zinatokana na Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo na TZS 150 bilioni ni Misaada ya Kibajeti).

**L.2 Mapendekezo ya Mgao wa Matumizi**

**183. Mheshimiwa Spik**a, Serikali inakadiria kutumia jumla ya **TZS 8,525.850 bilioni** zikiwemo:

**Matumizi ya Kazi za Kawaida TZS 2,737.480 bilioni** sawa na asilimia 32.1 ya makadirio ya bajeti yote ambayo yanajumuisha mambo yafuatayo:

i. **TZS 1,176.327 bilioni** Matumizi ya Mshahara;

ii. **TZS 634.890 bilioni** Matumizi ya Kuendeshea Ofisi;

iii. **TZS 573.171 bilioni,** Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali;

iv. **TZS 16.781 bilioni** Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani;

v**.** **TZS 336.311 bilioni** Matumizi kwa Taasisi zinazojitegemea.

**184. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Kazi za Maendeleo **TZS 5,788.370 bilioni** zimekadiriwa kutumika kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na asilimia 67.9 ya bajeti yote, zikiwemo:

i. **TZS 2,863.435 bilioni** Matumizi kwa Miradi Mipya ya kimkakati na inayoendelea kutoka Serikalini, **TZS 600.000 bilioni** kwa ajili ya mfuko wa kugharamia madeni na **TZS 970.363 bilioni** Miradi Mengineyo inayoendelea;

ii. **TZS 1,345.356 bilioni** Matumizi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo (TZS 1,105.251bilioni Mkopo, na TZS 240.105 bilioni ni Misaada); na

iii. **TZS 9.215 bilioni** Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Kiambatisho Namba:5.** Kinaonyesha mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa mujibu wa mapendekezo ya Sura ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## M. HALI YA UTEGEMEZI KWA MWAKA 2026/2027

185. **Mheshimiwa Spika,** Mageuzi yoyote katika nchi hutegemea uongozi wenye ubunifu, unaojituma na kusimama imara katika utekelezaji wa mikakati ya utoaji wa huduma na kuwatumikia wananchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 matarajio ya kiwango cha utegemezi wa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuendelea kupungua kutoka asilimia 4.9 iliyoripotiwa Mwaka 2025/2026 hadi kufikia asilimia 2.8 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kupungua huko kunatokana na kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mkakati wa Serikali wa kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Ndani.

## N. VIPAUMBELE VYA MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

186. **Mheshimiwa Spika,** Kwa utaratibu wetu, leo asubuhi nimewasilisha Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027, ambapo maeneo makuu manne tumeya ainisha, kwa muhutasari naomba nieleze maeneo hayo:-

**187. Mheshimiwa Spika,** Serikali imetenga jumla ya **TZS 3,797.39 bilioni**, kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi Mipya ya Kimkakati na ile inayoendelea, ambapo bajeti zao tayari tumeshapitisha katika Mafungu ya Wizara husika wakati tunapitisha bajeti za Wizara na Taasisi za Serikali yakiwemo:

**a.Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu**

**188. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu wezeshi ya usafiri wa anga, baharini na nchi kavu, kuimarisha nishati ya umeme na kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama, kuongeza ubora wa matumizi ya TEHAMA na huduma za kidijitali, na kuendeleza makaazi yanayozingatia muundo na haiba za miji.**TZS 1,733.838 bilioni** zitatumika sawa na asilimia 45.7 kwa ajili ya kutekeleza programu na miradi ifuatayo:

i. **TZS 554.500 bilioni** kwa ajili ya Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu zenye urefu wa kilomita 159.5;

ii. **TZS 254.721 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Ujenzi wa Barabara za Mjini, Ndani na Vijijini na uwekaji wa Taa za Barabarani;

iii. **TZS 269.079 bilioni** kutekeleza Programu ya Ujenzi wa Barabara zinazoingia katika Mji wa Michezo Fumba zenye urefu wa kilomita 63.8;

iv. **TZS 155.964 bilioni** kwa ajili ya Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar;

v. **TZS 210.500 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, Maegesho ya Ndege (Apron) na Jengo la Abiria Terminal II - Awamu ya Pili; na

vi. **TZS 289.074 bilioni** kwa ajili ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme.

**b. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

**189. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu na huduma za afya, elimu, na michezo, pamoja na mifumo ya hifadhi ya jamii. **TZS 1,257.927 bilioni** sawa na asilimia 33.1 zitatumika kutekeleza programu na miradi ifuatayo:

i. **TZS 666.068 bilioni** kwa ajili ya Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu;

ii. **TZS 186.872 bilioni** Ujenzi wa Kiwanja cha Michezo kilichopo Fumba (AFCON City);

iii. **TZS 300.920 bilioni** Ujenzi wa Nyumba za Makaazi za Kisakasaka, Chumbuni na Kikwajuni; na

iv. **TZS 104.067 bilioni** Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Binguni na Hospitali za Mikoa.

**c.Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi**

**190. Mheshimiwa Spika,** Serikali imetenga **TZS 643.94 bilioni** sawa na asilimia 17 kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza miundombinu ya bahari kuu, viwanda vya kusarifu mazao ya baharini, na utalii

wa bahari na visiwa, sambamba na kuimarisha kilimo cha biashara na usalama wa chakula pamoja na kuwezesha upatikanaji wa ajira za Serikali na Sekta Binafsi.

i. **TZS 65.000 bilioni** kwa ajili ya ujenzi wa Masoko;

ii. **TZS 64.544 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa kiwanda cha kuchakatia samaki na madiko ya kisasa;

iii. **TZS 10.460 bilioni** Ujenzi wa Miundombinu ya Uimarishaji wa zao la Mwani;

iv. **TZS 46 bilioni** Ujenzi wa Kituo cha kudumu cha kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia na Kufanya Utafiti wa Utafutaji wa Mafuta kwa Njia ya Mtetemo ya 3D;

v. **TZS 265.500 bilioni** Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani na Bandari ya Abiria Maruhubi;

vi. **TZS 40.025 bilioni** Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii, katika maeneo ya kihistoria na vivutio vya utalii;

vii. **TZS 115.213 bilioni** Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula na Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania; na

viii. **TZS 37.200 bilioni** Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo, Wakati na Wakubwa kwa kupatiwa mikopo.

**d. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**

**191. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki ili kuhakikisha nchi inaendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani sambamba na kukabiliana na mabadiliko ya

tabianchi. Kiasi cha **TZS 161.680 bilioni** sawa na asilimia 4.3 zitatumika kutekeleza programu na miradi ifuatayo:

i. **TZS 55.078 bilioni** Kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mji wa Serikali;

ii. **TZS 70.00 bilioni** kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha Kijeshi cha Kisasa cha Idara Maalum za SMZ; na

iii. **TZS 36.602 bilioni** kwa ajili ya Uboreshaji wa Mahkama za Mikoa na Wilaya.

## MWELEKEO WA BAJETI INAYOZINGATIA JINSIA NA USAWA KWA MWAKA 2026/2027

**192. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kuhakikisha kuwa maendeleo yanayopatikana yanawanufaisha wananchi wote kwa usawa, Serikali inaendelea kufanya mageuzi katika mfumo wa upangaji na utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia misingi ya usawa wa kijinsia. Mageuzi haya yanalenga kuhakikisha kuwa mahitaji, changamoto na fursa za wanawake, wanaume, vijana, watoto na makundi mengine maalumu yanazingatiwa ipasavyo katika mchakato mzima wa kupanga, kutenga na kutumia rasilimali za umma.

**193. Mheshiwa Spika,** Kwa Mwaka 2026/2027, Serikali imepanga kuimarisha utekelezaji wa Bajeti Inayozingatia Usawa wa Kijinsia (Gender Responsive Budgeting - GRB) kwa kuhusisha na kuainisha shughuli mahsusi zitakazotekelezwa kupitia miradi ya maendeleo pamoja na kuhakikisha kuwa matokeo ya miradi yanawanufaisha wananchi wote kwa usawa.

Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa taasisi za umma katika kuandaa, kufuatilia na kutathmini miradi kwa kutumia viashiria vinavyopima matokeo ya kijinsia, ili kuhakikisha kuwa kila shilingi inayowekezwa katika maendeleo inaleta manufaa jumuishi na endelevu kwa jamii. Kiasi cha **TZS 449.799 bilioni** zimepangwa kutumika katika maeneo mbalimbali ya kuimarisha jinsia na usawa katika jamii sawa na ongezeko la asilimia 525.4 ukilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita.

**194. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Serikali imeongeza Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji pamoja na kuongeza wigo kwa kutathmini Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa katika miradi ya maendeleo na hivyo kufanya wizara za majaribio kufikia tisa. Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuimarisha Huduma za mama na watoto wachanga na walio chini ya umri wa Miaka 5 pamoja na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za mkono kwa mkono (One Stop Center);
ii. Programu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto;
iii. Uimarishaji na usambazaji wa huduma za maji safi na salama;
iv. Kujenga skuli 2 za sekondari za wanawake kwa Mkoa wa Kusini Unguja na Mkoa wa Kusini Pemba ili kuimarisha upatikanaji wa fursa ya elimu ya Sekondari kwa watoto wa kike;

v. Kutayarisha vifaa vya utekelezaji wa mtaala rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na kununua na kusambaza vifaa saidizi;
vi. Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa wanawake, wanaume na watoto juu ya kupinga ukatili na udhalilishaji;
vii. Kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu;
viii. Kuwezesha wanawake kupata pembejeo, mikopo na masoko;
ix. Kuwajengea uwezo wanawake na vijana katika uzalishaji wa mazao ya vipaumbele vya mnyororo wa thamani (mihogo, ndizi, mwani na matango bahari) pamoja na kuwapatia mafunzo maafisa ugani kuhusu mbegu bora za mboga na matunda zinazostahamili mabadiliko ya tabianchi; na
x. Kufanya ukaguzi juu ya tatizo la ajira za watoto na watoto walio katika mazingira magumu kuwarejesha skuli.

## O. MGAWANYO WA SHUGHULI KUU ZA SERIKALI - COFOG

**195. Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa mageuzi ya bajeti ni matumizi ya Serikali kwa mujibu wa Mgawanyo wa Shughuli Kuu za Serikali (Classification of Functions of Government – COFOG). Mageuzi haya yanayoendelea ni nyenzo muhimu katika kuimarisha uwazi, ufanisi na upangaji wa rasilimali za umma kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya Taifa.

196. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa faida za Mfumo wa Mgawanyo wa Shughuli Kuu za Serikali ni:

i. Kuwezesha kulinganisha matumizi ya Serikali Kikanda na Kimataifa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya takwimu za fedha za umma;
ii. Husaidia kupanga, kuchambua na kufuatilia matumizi ya Serikali kwa kuzingatia kazi na huduma zinazotolewa kwa wananchi; na
iii. Huongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika ugawaji wa rasilimali za Serikali.

197. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2026/2027, Serikali imeelekeza rasilimali zake kwa kuzingatia mgawanyo wa shughuli kumi za Serikali (COFOG).Shughuli hizo zimegawika katika maeneo yafuatayo;

i. **Huduma za Jumla za Serikali (General Public Services**). Kundi hili linahusisha shughuli za utawala wa Serikali kwa ujumla ikiwemo usimamizi wa sera, mipango ya maendeleo, ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa fedha za umma, mahusiano ya kimataifa, huduma za kidiplomasia pamoja na usimamizi wa taasisi za Serikali. Pia linajumuisha gharama za uendeshaji wa mihimili ya Serikali na ulipaji wa deni la Taifa;
ii. **Masuala ya Uchumi** (**Economic Affairs**). Hili ni kundi linalojumuisha sekta zinazochochea ukuaji wa uchumi kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, biashara, viwanda, utalii, uchukuzi, mawasiliano, nishati na maendeleo ya miundombinu ya kiuchumi;

iii. **Elimu (Education),** inajumuisha elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya kati na elimu ya juu pamoja na mafunzo ya ufundi na elimu maalum. Pia linahusisha maendeleo ya miundombinu ya elimu, mitaala na kuongeza ubora wa elimu;

iv. **Makazi na Huduma za Jamii** (**Housing and Community Amenities**), Kundi hili linajumuisha upangaji wa miji, maendeleo ya makazi, huduma za maji safi na usafi wa mazingira, taa za barabarani pamoja na maendeleo ya jamii katika maeneo ya mijini na vijijini;

v. **Afya (Health)**, inajumuisha huduma zote za afya ikiwemo hospitali, vituo vya afya, zahanati, kinga na tiba, huduma za mama na mtoto, upatikanaji wa dawa, pamoja na programu za kudhibiti magonjwa na kuimarisha afya ya jamii;

vi. **Usalama na Utulivu wa Jamii** (**Public Order and Safety)**, kundi hili linahusisha shughuli za magereza, zimamoto, mahakama pamoja na taasisi zinazohakikisha utekelezaji wa sheria, usalama wa wananchi na utulivu wa jamii;

vii. **Ulinzi** (**Defence**), linajumuisha shughuli zinazohusu ulinzi wa Taifa, mafunzo ya ulinzi pamoja na shughuli za kulinda mipaka, na bahari;

viii. **Burudani, Utamaduni na Dini** (**Recreation, Culture and Religion**), kundi hili linahusisha maendeleo ya michezo, sanaa, utamaduni, makumbusho, maktaba, shughuli za vijana pamoja na uhifadhi wa urithi wa Taifa na maeneo ya kihistoria;

ix. **Hifadhi ya Jamii (Social Protection)**. Kundi hili linajumuisha huduma za ustawi wa jamii kwa makundi maalum kama watoto, wazee, watu wenye ulemavu na kaya zisizojiweza, misaada ya kijamii na programu za kupunguza umaskini; na

**x. Hifadhi ya Mazingira (Environmental Protection)** Linahusisha shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwemo usimamizi wa taka, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, uhifadhi wa misitu, usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

## P. MAZINGATIO YA MATUMIZI KATIKA MAENEO MAALUM KULINGANA NA SERA ZA MATUMIZI KWA BAJETI YA 2026/2027

**198. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Serikali inaendelea na Mageuzi mbalimbali ya kisera katika maeneo ambayo yataimarisha ukusanyaji wa mapato na kuimarisha hali ya kiuchumi Zanzibar.Katika mwaka wa fedha ujao, Serikali itaendelea kuimarisha nidhamu ya matumizi fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa rasilimali zilizopo zinatumika kwa ufanisi,tija na kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money). Miongoni mwa maeneo yaliyozingatiwa ni:

i Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa karibu na kuhakikisha matumizi yote yanaendana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

ii. Kufuatia fursa ya uwepo wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2027 (Africa Cup of Nations-AFCON 2027), Serikali imetenga kiasi cha **TZS 1,069.754 bilioni** kwa ajili ya uwekezaji na kuimarisha maandalizi ya kitaifa katika miundombinu ya michezo, usafiri, utalii na huduma za kijamii, kwa lengo la kutumia mashindano hayo kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi, ajira na utangazaji wa Taifa kimataifa;
iii. **TZS TZS 449.799 bilioni** zimepangwa Kuimarisha Ujumuishaji wa Usawa wa Kijinsia katika Miradi ya Maendeleo, kwa kuhusisha na kuainisha shughuli pamoja na matokeo yanayolengwa katika utekelezaji wa miradi hiyo, hatua itakayowezesha rasilimali za umma kutumika kwa ufanisi zaidi na kuhakikisha manufaa ya maendeleo yanawafikia wananchi wote kwa usawa;
iv. Serikali imetenga **TZS 400.920 bilioni** kwa ajili ya Uwekezaji kwa Taasisi tatu (3) za Serikali ikiwemo, Kampuni ya Mwani - ZASCO TZS 30 bilioni, Kamisheni ya Utalii TZS 70 bilioni na Shirika la Nyumba **TZS 300.920 bilioni;**
v. Serikali imetenga **TZS 290 bilioni** kwa ajili ya nafasi za ajira mpya na nyongeza ya mshahara na maslahi mengine ya watumishi wa umma;
vi. Serikali imetenga **TZS 167.868 bilioni** kutoka Kodi ya Mfuko wa Miundombinu kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi maalum ya maendeleo, ambapo jumla ya wizara tatu (3) baadhi ya miradi yake imepangiwa kutumia fedha hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa

matumizi ya Mfuko huo. Miradi iliyopangwa kwa fedha hizo imeambatishwa;

vii. **TZS 27.368 bilioni** zimetengwa kutoka Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi (SDL) kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Uimarishaji wa Elimu ya juu kupitia mkopo wa elimu ya juu na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia sambamba na kuimarisha karakana za kufundishia na kujifunzia kwa kuzipatia vifaa na mashine za kisasa;

viii. **TZS 2.800 bilioni** zimetengwa kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo kwa wakulima ikiwemo (mbolea, madawa na mbegu);

ix. Kuziwezesha sekta za uzalishaji na ukusanyaji wa mapato ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani.

**199. Mheshimiwa Spika,** Katika dhamira ya kuendelea kuimarisha ustawi wa watumishi wa umma na kutambua mchango wao mkubwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, imeendelea kuweka maslahi ya watumishi kuwa miongoni mwa vipaumbele muhimu vya utekelezaji wa sera za maendeleo ya Taifa.

**200. Mheshimiwa Spika,** Tukumbuke kuwa wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** alitangaza ongezeko la Mishahara kwa kima cha chini kutoka Shilingi laki tatu (300,000) hadi kufikia shilingi laki tano (500,000). Hatua hii ni kielelezo cha dhamira thabiti ya Serikali ya kuhakikisha kwamba

matunda ya ukuaji wa uchumi yanawafikia wananchi moja kwa moja kupitia watumishi wa umma ambao ndio nguzo kuu ya utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo.

201. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuhamasisha ari ya utendaji, kuongeza tija katika utumishi wa umma na kuboresha hali ya maisha ya watumishi. Mheshimiwa Rais **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** ametuelekeza kuwa marekebisho ya mishahara ya watumishi wote kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi (Scheem of Services) yaanze kutekelezwa mara tu baada ya kukamilika Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kwa mantiki hiyo, Mishahara mipya kwa watumishi wote itaanza kulipwa mwezi wa Oktoba 2026, **badala** ya Robo ya Tatu (inayoanzia Januari 2027) iliyokuwa imepangwa awali.

## Q. SHUKURANI

202. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa **Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa uongozi wake mahiri unaoendelea kuimarisha misingi ya amani, utulivu, mshikamano na haki nchini. Dhamira yake ya kusimamia maridhiano, utawala bora na maendeleo jumuishi imeendelea kuifanya Tanzania kuwa nchi ya amani na matumaini kwa wananchi wake. Kupitia mwenendo wake wa hekima, ameendelea kuwa mfano wa kuigwa katika kuimarisha tunu za jamii na kusaidia mazingira bora ya utekelezaji wa majukumu ya uongozi wa juu wa nchi.

**203. Mheshimiwa Spika**, Aidha, tunatoa pongezi na shukurani za dhati kwa mume wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mzee wetu Hafidh Ameir, kwa mchango wake wa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kitaifa. Uungwaji mkono wake umeendelea kudhihirisha uzalendo, maadili mema na mshikamano wa kifamilia unaoimarisha heshima na taswira ya uongozi wa Taifa.

**204. Mheshimiwa Spika**, Kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na pia kuniteua kushika dhamana ya Waziri wa Fedha na Mipango. Imani hii kubwa niliyopewa sio tu heshima bali ni jukumu linalonipa wajibu wa kulitumikia Taifa letu kwa bidii zaidi, uadilifu na uzalendo wa hali ya juu. Naahidi kuendelea kusimamia rasilimali za umma kwa umakini mkubwa, kuhakikisha uwajibikaji, pamoja na kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali ili kufanikisha malengo ya maendeleo ya Zanzibar. Niahidi mbele ya wajumbe wako nitaitumikia nafasi hii kwa uweledi, busara na maarifa yangu yote kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyo niwafikisha kuyatekeleza, **namuomba Mola wangu Mtukufu anisaidie.**

**205. Mheshimiwa Spika,** Historia ya Maendeleo ya sekta ya Fedha na Mipango Zanzibar, itaendelea kutambua mchango mkubwa wa Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** si kwa

nafasi aliyoishika pekee, bali kwa mabadiliko aliyoyaleta, dira aliyotoa na matumaini aliyoyapanda katika mioyo ya Wazanzibari. Sisi tuliopata fursa ya kufanya kazi chini ya uongozi wake tutaendelea kuthamini mchango wake katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya fedha za umma na Maendeleo ya Uchumi wa Zanzibar. **Mheshimiwa Spika, Baadhi ya Viongozi huacha kumbukumbu za madaraka yao, lakini viongozi wa aina yake huacha alama za uongozi wao katika mioyo ya watu.**

**206.** **Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Rais **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** ameendelea kuthibitisha kuwa uongozi bora si suala la kuongoza taasisi pekee, bali ni uwezo wa kubadilisha maisha ya watu. Kila mradi unaotekelezwa, kila huduma inayoboreshwa na kila hatua ya Maendeleo inayoshuhudiwa leo ni ushahidi wa maono yake na dhamira yake ya kuwatumikia wananchi. Tunapomshukuru, hatumshukuru kwa sababu ya nafasi yake ya Urais pekee, bali tunamshukuru kwa kuwa kiongozi aliyetoa matumaini pale palipokuwa na changamoto, aliyetoa dira pale palipohitajika mwelekeo na aliyeendelea kuamini kuwa Zanzibar inaweza kufikia mafanikio makubwa zaidi. Mungu amlinde, ampe afya njema na aendelee kumjalia hekima katika kuiongoza Zanzibar yetu.

**207.** **Mheshimiwa Spika,** Pongezi kwa mama yetu, Mama Maryam Mwinyi, mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali**

**Mwinyi,** kwa mchango wake mkubwa katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais kupitia shughuli za kijamii na maendeleo zinazotekelezwa na taasisi ya ***Zanzibar Maisha Bora Foundation.*** Kupitia juhudi zake, Mama Maryam ameendelea kugusa maisha ya makundi mbalimbali ya jamii hususan wanawake, vijana na watoto, kwa kuhamasisha ustawi wa jamii, elimu, afya na mshikamano wa kijamii. Ushiriki wake umeendelea kuwa chachu muhimu ya kuimarisha jitihada za Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo na matumaini. Sambamba na hilo mama yetu ni mlezi mzuri kwa kiongozi wetu wa nchi, hakika ulezi tuliomkabidhi amekuwa akiutunza vyema na matunda ya malezi yake yamekuwa yakitoa matokeo chanya na chachu ya kuwaletea wananchi wetu maendeleo.

**208. Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima kubwa, tunampongeza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla, kwa uongozi wake mahiri, busara na miongozo yake yenye dira katika kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi. Uwezo wake wa kuongoza kwa hekima, kujenga mshikamano na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa weledi, umeendelea kuwa chachu ya kuimarisha utendaji, uwajibikaji na mafanikio ya Serikali katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. Maono yake na uzalendo wake vimeendelea kutoa mwelekeo imara katika kuimarisha misingi ya utawala bora na ustawi wa wananchi.

**209. Mheshimiwa Spika,** Kipekee nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi. Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa **Zubeir Ali Maulid,** ukiwa kiongozi mbobezi wa kusimamia Muhimili huu wa Baraza la kutunga Sheria (BLW) kwa namna ulivyoongoza shughuli za Baraza hili kwa hekima, weledi na ustahimilivu mkubwa. Aidha, nawapongeza wasaidizi wako wote wakiwemo; Naibu Spika Mheshimiwa **Mwanaasha Khamis Juma**, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili kwa michango yao yenye kujenga ushirikiano na ushauri uliowezesha kujadili na kuboresha hoja zilizowasilishwa kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla.

**210. Mheshimiwa Spika,** Natoa shukurani mahsusi kwa Kamati ya Bajeti, chini ya uongozi wa Mheshimiwa **Ali Suleiman Ameir (Mrembo)**. Kwa hakika, wametujengea uwezo mkubwa sana, mimi binafsi pamoja na watendaji wangu, tunaendelea kufaidika na miongozo yao. Kupitia Kamati hii, watendaji wetu wameongeza weledi na umakini katika kutekeleza majukumu yao.

**211. Mheshimiwa Spika**, Nitoe pongezi kwa Msaidizi wangu wa karibu, Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa **Dkt. Hamad Bakar Hamad**, kwa kweli amekuwa kiungo muhimu katika Wizara yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa siha, busara na ujasiri katika kutekeleza majukumu yake. Hakika wananchi wa Micheweni hawakukosea kumchagua Mheshimiwa Hamad

kutokana na uamuzi wake wa dhati wa kuibeba dhamana hiyo kama ni deni kwa taifa lake.

**212.** **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za dhati, kwa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Mheshimiwa **Dkt. Saada Mkuya Salum,** kwa uongozi wake mahiri, na mchango wake mkubwa katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na maendeleo ya uchumi wa Zanzibar. Katika kipindi cha uongozi wake, alitoa miongozo, maelekezo na ushauri wenye busara ulioweka msingi imara wa nidhamu ya fedha, uwajibikaji na ufanisi katika utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo. Kwa niaba ya Wizara, tunamtakia afya njema, mafanikio makubwa na baraka tele katika majukumu yake ya sasa

**213.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba uniruhusu nitoe pongezi na shukurani zangu kwa viongozi wote wa vyama vyote walioteuliwa na waliochaguliwa na kuaminiwa kuweza kuingia katika chombo hichi muhimu cha kutunga Sheria.

**214.** **Mheshimiwa Spika**, Hakika sisi sote ni wamoja, na tunasafiri kwa safina moja inayoongozwa na nahodha mmoja nae ni Dkt. **Hussein Ali Mwinyi**, kwa pamoja tunatakiwa kuhakikisha kuwa, kwa jasho na damu zetu tunakifikisha chombo chetu salama kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi. ***Tofauti zetu za maoni zisigeuke kuwa chanzo cha mgawanyiko, bali zitumike kama nguvu ya kuimarisha demokrasia na kuharakisha maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake.***

**215. Mheshimiwa Spika,** Naomba niendelee kutoa wito kwa viongozi wenzangu na wananchi wote kwa ujumla kuwa uchaguzi umekwisha na sasa ni wakati wa kuendeleza mshikamano, kuimarisha maridhiano na kuelekeza nguvu zetu katika ujenzi wa Taifa letu. Hivyo, viongozi wa kisiasa na wananchi kwa ujumla wanahimizwa kuweka mbele maslahi ya nchi, kudumisha amani na utulivu, pamoja na kushirikiana katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ustawi wa Taifa letu.

**216. Mheshimiwa Spika**, Sitaitendea haki hotuba yangu bila kutoa pongezi kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini yake, wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu na Naibu Katibu CPA(T) **Aboud Hassan Mwinyi.** Kwa hakika Ndg. Aboud amekuwa akizitumikia vyema nafasi zake licha ya majukumu mazito anayoyatekeleza kwa sasa kama Mlipaji Mkuu wa Serikali. Namshukuru na kumpongeza Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango **Dkt. Afua Khalfan Mohamed**, Mhasibu Mkuu wa Serikali CPA(T) **Hamad Saleh Hamad**, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar CPA(T) **Said Kiondo Athumani** na Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar **Ndg. Saleh H. Pandu.** pamoja na watendaji wote kwa mashirikiano na mshikamano wao wa dhati. Nawashukuru kwa dhati Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Ofisi yangu. Kipekee kabisa, namshukuru na kumpongeza Kamishna wangu wa Bajeti **Ndg. Zena Mahmoud Hassan** na watumishi wote walio chini

ya Idara hiyo na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kazi kubwa wanazozifanya na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**217. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kutoa shukurani za dhati kwa familia yangu kwa kuendelea kuniombea na kuniunga mkono katika nyakati za kutekeleza majukumu mazito ya Serikali, mchango wao mkubwa, uvumilivu na ushirikiano wanaoendelea kunipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa umekuwa ni nguvu muhimu inayoniwezesha kulitumikia taifa letu kwa bidii na uadilifu. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**218. Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini, kunilea kisiasa na kunipa fursa adhimu ya kulitumikia Taifa kupitia uteuzi wa nafasi mbalimbali za uongozi nilizowahi na ninazoendelea kupewa. Imani hii siichukulii kama heshima binafsi pekee, bali ni dhamana kubwa inayonipa wajibu wa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo. Ninachoweza kukiahidi Chama Changu na wananchi wa Zanzibar ni kwamba imani hii waliyoendelea kunipa haitapotea bure, itaonekana katika utendaji wangu, itaonekana katika matokeo ya kazi zangu, na itaendelea kuonekana katika mchango wangu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**219. Mheshimiwa Spika,** Tunapenda kutoa shukurani za dhati na za pekee kwa nchi Marafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Kimataifa, Jumuiya za Kikanda, Taasisi za

Kiserikali pamoja na Wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuchangia Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 Miongoni mwao ni: Germany, Japan, JICA, Norway, EXIM Bank, India, South Korea, Oman, United Arab Emirates, African Development Bank (AfDB), European Union (EU), Global Fund, United National Development Program (UNDP),WHO, UNICEF, FAO,BADEA , IFAD, OPEC, UNEP, UN Women, UNFPA , Health Improvement Programme in Zanzibar (HIPZ), UK , Global Alliance for Vaccines and Immunization (GAVI), BASKET FUND, Adaptation Fund, COSTECH, World Bank, STBF, IRISH EMBASSY, DLI, GPE, KFW, QUEEN'S BELFAST UNIVERSITY, SAUDI FUND, BADEA,UKEF, DEUTSCHE BANK, CITI BANK, KOICA, AUSTRIA, Exim Bank Korea, NETHERLAND, Nutritional International (NI) ,UN-AIDS , GEF, UNCDF, WORLD BANK, Foreign Common Wealth and Development Office , BIG WIN PHILANTHROPY UK , GATE Foundation, Vital Strategies Data for Health ,,CDC (Center for disease control, Center for international Health Education , Vital Strategies (USA) and Biosecurity (CIHEB), Commonwealth of Learning (COL).

## R. HITIMISHO

220. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato ya Serikali ya kukusanya TZS 8,525.850 bilioni (Shilingi Trilioni Nane, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Nane na Hamsini).

Kati ya mapato hayo, TZS 8,163.543 bilioni Makusanyo ya Serikali Kuu. Kwa upande wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni TZS 25.996 bilioni na Taasisi za Serikali zinazojitegemea ni TZS 336.311 bilioni, naliomba Baraza lako tukufu kuridhia makusanyo hayo kupitia Mamlaka zao.

**221. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, tunaliomba Baraza lako liidhinishe **TZS 8,525.850 bilion**i (Shilingi Trilioni Nane, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Nane na Hamsini), kati ya hizo **TZS 2,737.480 bilioni** kwa ajili ya kazi za kawaida, (zinajumuisha TZS 16.781 bilioni za Mamlaka za Serikali za Mitaa na TZS 336.311 bilioni za Taasisi za Serikali Zinazojitegemea). **TZS 5,788.370 bilioni** zimeelekezwa kwenye kutekeleza Mpango wa Maendeleo (zinajumuisha **TZS 9.215 bilioni** za Mamlaka za Serikali za Mitaa).

**222. Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja.



***DKT. JUMA MALIK AKIL (MBM)***
***WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO,***
***ZANZIBAR.***

***JUN1, 2026.***

## S. VIAMBATISHO

| | |
|---|---|
| **Kiambatisho Namba:1** | Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali Julai 2025, hadi Machi, 2026, |
| **Kiambatisho Namba:2** | Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Julai 2025, hadi Machi, 2026, |
| **Kiambatisho Nama: 3** | Utekelezaji wa Bajeti kwa Taasisi zinazojitegemea Julai 2025, hadi Machi ,2026, |
| **Kiambatisho Namba:4** | Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi kufikia Juni 2026, |
| **Kiambatisho Namba:5** | Sura ya Bajeti Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 |
| **Kiambatisho Namba:6** | Mfumo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 hadi 2028/2029 Makadirio ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 hadi 2028/2029 |

| Kiambatisho Namba :1 UTEKELEZAJI WA BAJETI KIPINDI CHA JULAI 2025- MACHI, 2026 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Halisi Julai - Machi 2024/25 | Bajeti 2025/26 | Makadirio Julai-Machi 2025/26 | Halisi Julai-Machi 2025/26 | %Bajeti | % Julai - Machi | %Ukuaji |
| **MAPATO** | | | | | | | |
| **Mapato ya Serikali Kuu** | **2,064.50** | **6,622.68** | **3,346.89** | **3,386.10** | **51.13** | **101.17** | **64.02** |
| **Mapato ya Kodi** | **1,142.32** | **2,104.01** | **1,497.42** | **1,463.43** | **69.55** | **97.73** | **28.11** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,710.94** | **5,177.84** | **2,857.58** | **2,814.36** | **54.35** | **98.49** | **64.49** |
| ZRA | 655.53 | 1,257.24 | 878.58 | 826.97 | 65.78 | 94.13 | 26.15 |
| TRA | 471.04 | 825.77 | 603.10 | 620.70 | 75.17 | 102.92 | 31.77 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 150.15 | 293.83 | 204.82 | 167.13 | 56.88 | 81.60 | 11.31 |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 15.75 | 21.00 | 15.75 | 15.75 | 75.00 | 100.00 | 0.00 |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | ***10.33*** | ***21.67*** | ***13.46*** | ***12.87*** | ***59.38*** | ***95.60*** | ***24.56*** |
| ***Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)*** | ***129.54*** | ***337.73*** | ***261.26*** | ***234.90*** | ***69.55*** | ***89.91*** | ***81.34*** |
| **Mapato ya Washirika wa Maendeleo** | **353.56** | **1,444.84** | **489.31** | **571.74** | **39.57** | **116.85** | **61.71** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 76.58 | 120.00 | 62.27 | 79.48 | 66.23 | 127.64 | 3.79 |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.27 | 0.54 | 0.45 | 0.51 | 94.71 | 113.44 | 87.68 |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 51.44 | 361.56 | 69.46 | 69.46 | 19.21 | 99.99 | 35.03 |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta | 225.27 | 962.74 | 357.13 | 422.30 | 19.21 | 118.25 | 87.46 |
| **Mkopo wa Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** | **418.47** | **2,780.00** | **1,155.34** | **1,183.80** | **42.58** | **102.46** | **182.89** |
| Mkopo wa ndani | 283.47 | 1,080.00 | 784.97 | 813.44 | 75.32 | 103.63 | 186.96 |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 135 | 1,700.00 | 370.37 | 370.37 | 21.79 | 100.00 | 174.34 |
| **JUMLA YA MAPATO ( Serikali kuu +LGA+OunSource)** | **2,204.37** | **6,982.077** | **3,621.61** | **3,633.87** | **52.05** | **100.34** | **64.85** |
| **MATUMIZI** | | | | | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | **1,208.46** | **2,433.27** | **1,694.59** | **1,646.21** | **67.65** | 97.14 | 36.22 |
| Mshahara Mawizara | 489.07 | 810.93 | 504.81 | 500.30 | 61.70 | 99.11 | 2.30 |
| Mshahara Ruzuku | 94.25 | 142.81 | 101.37 | 101.48 | 71.06 | 100.11 | 7.67 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 164.7 | 482.08 | 222.94 | 217.56 | 45.13 | 97.59 | 32.09 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 49.35 | 108.89 | 67.08 | 64.00 | 58.78 | 95.41 | 29.69 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 284.6 | 538.34 | 557.33 | 561.58 | 104.32 | 100.76 | 97.32 |
| ***Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | ***9.84*** | ***12.50*** | ***9.52*** | ***10.23*** | ***81.87*** | ***107.50*** | ***4.00*** |
| ***Matumizi ya Taasisi zinazojitegemea*** | ***116.65*** | ***337.73*** | ***231.53*** | ***191.05*** | ***56.57*** | ***82.52*** | ***63.78*** |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **1,174.69** | **4,548.81** | **1,711.81** | **1,770.09** | **38.91** | **103.40** | **50.69** |
| Fedha za Serikali | 858.4 | 2,919.40 | 933.82 | 1,414.53 | 48.45 | 151.48 | 64.79 |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo | 162.78 | 312.00 | 347.34 | 304.69 | 97.66 | 87.72 | 87.18 |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 34.14 | 345.50 | 69.46 | 100.79 | 29.17 | 145.10 | 195.22 |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 117.79 | 962.74 | 357.13 | 253.95 | 26.38 | 71.11 | 115.60 |
| Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1.58 | 9.17 | 4.07 | 0.82 | 8.90 | 20.05 | -48.35 |
| **JUMLA YA MATUMIZI ( Serikali kuu +LG** | **2,383.15** | **6,982.076** | **3,406.40** | **3,416.30** | **48.93** | **100.29** | **43.35** |
| ***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango*** | | | | | | | |

| Kiambatisho Namba :2 UTEKELEZAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **MAPATO** | | | |
| **TAASISI** | **Makadirio Julai Machi 2025/2026** | **Halisi Julai 2025 hadi Machi 2026** | **Asilimia** |
| Baraza la Manispaa Mjini | 2,462,777,500 | 2,154,896,037 | 87% |
| Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 1,777,163,364 | 2,219,020,281 | 125% |
| Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 2,173,105,668 | 1,802,881,401 | 83% |
| Baraza la Manispaa Kaskazini"A" | 2,112,248,865 | 1,871,471,977 | 89% |
| Baraza la Mji Kaskazini "B" | 1,193,829,000 | 874,872,852 | 73% |
| Baraza la Manispaa Kati | 1,355,000,000 | 1,061,107,761 | 78% |
| Baraza la Mji Kusini | 696,890,535 | 1,156,198,670 | 166% |
| Baraza La Manispaa Chake Chake | 660,772,650 | 621,795,075 | 94% |
| Baraza la Mji Mkoani | 311,647,187 | 464,932,437 | 149% |
| Baraza la Mji Wete | 376,733,001 | 325,510,925 | 86% |
| Halmashauri ya Wilaya Micheweni | 340,000,000 | 314,717,956 | 93% |
| **JUMLA** | **13,460,167,770** | **12,867,405,372** | **96%** |
| **MATUMIZI** | | | |
| **TAASISI** | **Makadirio Julai Machi 2025/2026** | **Halisi Julai 2025 hadi Machi 2026** | **ASILIMIA** |
| Baraza la Manispaa Mjini | 2,405,840,509 | 2,220,505,135 | 92% |
| Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 1,777,163,364 | 2,338,488,102 | 132% |
| Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 2,590,980,363 | 1,966,545,008 | 76% |
| Baraza la Manispaa Kaskazini"A" | 1,430,692,807 | 926,533,709 | 65% |
| Baraza la Mji Kaskazini "B" | 1,287,439,150 | 766,881,815 | 60% |
| Baraza la Manispaa Kati | 1,355,000,000 | 769,666,328 | 57% |
| Baraza la Mji Kusini | 1,126,760,535 | 751,849,703 | 67% |
| Baraza La Manispaa Chake Chake | 659,257,001 | 442,298,101 | 67% |
| Baraza la Mji Mkoani | 454,427,790 | 451,196,790 | 99% |
| Baraza la Mji Wete | 304,085,100 | 228,926,941 | 75% |
| Halmashauri ya Wilaya Micheweni | 197,759,282 | 186,659,282 | 94% |
| **JUMLA** | **13,589,405,901** | **11,049,550,914** | **81%** |
| *Chanzo: OR Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, 2026* | | | |

**Kiambatisho Namba :3 UTEKELEZAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**

| No. | JINA LA TAASISI | MAKADIRIO YA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA MAPATO JULAI-MACHI, 2025/2026 | HALISI JULAI - MACHI, 2025/2026 | ASILIMIA | MAKADIRIO YA MATUMIZI JULAI - MACHI, 2025/2026 | HALISI JULAI - MACHI,2025/2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali -(BPRA) | 5,000,000,000 | 3,900,800,000.00 | 5,702,587,134.00 | 146% | 3,590,233,123.00 | 3,046,365,286.00 | 85% |
| 2 | Afisi ya Msajili Wa Hakimiliki Zanzibar-(COSOZA) | 225,034,000 | 327,267,000.00 | 235,592,000.00 | 72% | 327,267,000.00 | 235,592,000.00 | 72% |
| 3 | Skuli ya Sheria Zanzibar -(LSZ) | 199,600,000 | 165,450,000.00 | 88,774,000.00 | 54% | 185,735,000.00 | 41,770,000.00 | 22% |
| 4 | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 462,000,000 | 429,000,000.00 | 424,425,000.00 | 99% | 429,000,000.00 | 357,851,886.48 | 83% |
| 5 | Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar | 1,500,000,000 | 1,133,865,998.00 | 748,987,908.00 | 66% | 1,141,653,997.00 | 845,501,641.70 | 74% |
| 6 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar-(ZURA) | 34,666,695,809 | 29,383,318,340.00 | 23,698,791,455.00 | 81% | 29,918,147,788.43 | 27,358,212,326.37 | 91% |
| 7 | Shirika la Utangazaji Zanzibar -(ZBC) | 5,432,440,000 | 2,280,094,656.00 | 2,219,100,999.04 | 97% | 2,280,094,656.00 | 2,143,542,631.04 | 94% |
| 8 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar -(BTMZ) | 391,492,000 | 8,100,000.00 | 360,000.00 | 4% | 8,100,000.00 | 360,000.00 | 4% |
| 9 | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo Zanzibar | 1,214,000,000 | 926,750,000.00 | 747,519,595.00 | 81% | 479,651,500.00 | 369,330,142.00 | 77% |
| 10 | Kamisheni ya Utalii Zanzibar | 12,527,262,900 | 10,485,897,081.00 | 9,238,217,666.02 | 88% | 7,797,711,804.00 | 6,216,321,745.00 | 80% |
| 11 | Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia Zanzibar -(KIST) | 38,220,350,529 | 2,311,871,000.00 | 1,377,485,208.00 | 60% | 2,230,526,000.00 | 1,515,391,066.00 | 68% |
| 12 | Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu Zanzibar -(ZHELB) | 5,694,400,000 | 4,667,125,000.00 | 4,099,031,045.00 | 88% | 4,667,125,000.00 | - | 0% |
| 13 | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi Zanzibar | 1,740,598,650 | 1,415,791,400.00 | 939,888,200.00 | 66% | 770,973,000.00 | 440,693,629.80 | 57% |
| 14 | Chuo cha Utawala wa Umma-(IPA) | 3,107,300,000 | 2,859,535,000.00 | 2,112,268,652.00 | 74% | 3,211,393,000.00 | 1,966,458,967.00 | 61% |
| 15 | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | 6,651,013,000 | 4,633,486,350.00 | 3,884,370,889.00 | 84% | 4,633,486,350.00 | 4,319,731,227.00 | 93% |
| 16 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar -(ZGP) | 1,082,687,232 | 6,320,299,375.50 | 3,700,015,818.74 | 59% | 6,240,525,388.00 | 5,287,500,657.95 | 85% |
| 17 | Taasisi ya Viwango Zanzibar -(ZBS) | 6,000,000,000 | 4,933,384,500.00 | 9,494,058,016.69 | 192% | 6,869,342,324.05 | 9,018,371,783.06 | 131% |
| 18 | Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar-(ZFDA) | 3,293,169,277 | 2,458,719,994.00 | 2,294,904,797.53 | 93% | 2,211,046,174.93 | 1,926,642,458.74 | 87% |
| 19 | Tume ya Utangazaji | 420,000,000 | 311,100,000.00 | 139,600,000.00 | 45% | 197,200,000.00 | 90,720,000.00 | 46% |
| 20 | Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege -(ZAA) | 49,778,922,218 | 43,604,183,256.48 | 39,485,725,262.03 | 91% | 43,273,714,652.00 | 40,012,770,587.03 | 92% |
| 21 | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar-(ZMA) | 9,111,534,121 | 6,607,774,222.00 | 5,868,704,254.00 | 89% | 6,263,598,986.00 | 2,746,143,996.00 | 44% |
| 22 | Mamlaka ya Mapato Zanzibar-(ZRA) | 2,598,000,000 | 1,810,000,000.00 | 2,057,000,000.00 | 114% | 1,065,000,000.00 | 1,004,000,000.00 | 94% |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shirika la Mawasiliano Zanzibar-(ZICTIA) | 18,206,627,080 | 11,623,030,125.00 | 8,630,012,514.76 | 74% | 11,273,491,570.00 | 8,418,309,376.18 | 75% |
| Mamlaka ya Maji Zanzibar-(ZAWA) | 10,924,843,656 | 3,932,726,421.64 | 1,711,195,141.16 | 44% | 3,932,726,421.64 | 1,711,195,141.16 | 44% |
| Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji-(ZIPA) | 3,731,722,570 | 3,303,647,033.68 | 4,886,000,085.33 | 148% | 3,637,581,688.00 | 3,829,564,131.32 | 105% |
| Chuo Kikuu Cha Taifa-(SUZA) | 16,088,190,900 | 13,572,963,508.00 | 9,660,392,525.00 | 71% | 15,291,480,040.00 | 9,515,943,191.41 | 62% |
| Kamisheni ya Ardhi | 10,164,108,136 | 7,536,558,615.00 | 5,994,176,592.00 | 80% | 4,469,878,820.00 | 2,056,229,931.33 | 46% |
| Mamlaka ya Mafunzo ya Amali -(VTA) | 45,384,121,050 | 372,525,534.00 | 188,621,864.00 | 51% | 760,525,534.00 | 159,579,937.00 | 21% |
| Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti | 431,550,000 | 267,800,000.00 | 239,735,000.00 | 90% | 267,800,000.00 | 239,735,000.00 | 90% |
| Chuo Kikuu cha Kiislamu | 1,589,152,600 | 1,191,864,450.00 | 533,590,846.00 | 45% | 1,191,864,450.00 | 543,871,419.64 | 46% |
| Idara ya Nishati na Madini | 15,420,700,000 | 15,560,974,500.00 | 15,152,667,635.25 | 97% | 15,560,974,500.00 | 15,152,667,635.25 | 97% |
| Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | 3,600,000,000 | 2,690,255,000.00 | 2,529,362,043.99 | 94% | 2,690,255,000.00 | 2,529,362,043.99 | 94% |
| Taasisi ya Elimu Zanzibar | 50,000,000 | 221,295,000.00 | 312,615,000.00 | 141% | 221,295,000.00 | 259,547,000.00 | 117% |
| Viwanda vya Idara Maalum za SMZ | 900,000,000 | 360,000,000.00 | 164,144,166.00 | 46% | 360,000,000.00 | 164,144,166.00 | 46% |
| Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima | 97,900,000 | 138,191,115.72 | 52,667,827.20 | 38% | 138,191,115.72 | 52,667,827.20 | 38% |
| Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 1,060,000,000 | 911,200,000.00 | 1,060,909,295.80 | 116% | 906,900,000.00 | 1,108,608,162.62 | 122% |
| Wakala wa Ulinzi JKU | 2,898,417,983 | 6,837,264,000.00 | 4,318,586,904.11 | 63% | 5,110,464,000.00 | 3,129,288,687.89 | 61% |
| Kamisheni ya Kazi | 1,800,000,000 | 5,125,132,321.00 | 4,819,113,207.00 | 94% | 3,275,238,848.00 | 2,971,895,407.00 | 91% |
| Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar | 300,000,000 | 3,147,314,250.00 | 2,222,767,523.24 | 71% | 1,030,000,000.00 | 844,089,788.49 | 82% |
| Wakala wa Barabara Zanzibar | 42,640,000 | 26,109,546.75 | 21,826,677.96 | 84% | 26,109,546.75 | 8,393,334.00 | 32% |
| Idara ya Misitu | 3,135,238,000 | 2,291,243,369.00 | 1,396,684,065.41 | 61% | 2,291,243,369.00 | 1,396,684,065.41 | 61% |
| Kampuni ya Uvuvi | 1,471,250,000 | 971,550,000.00 | 486,827,000.00 | 50% | 735,265,250.00 | 632,447,239.00 | 86% |
| Kampuni ya Mwani | 11,011,032,240 | 45,708,000,000.00 | 51,012,000,000.00 | 112% | 23,431,577,649.36 | 26,480,367,810.96 | 113% |
| **Jumla** | **337,726,868,950** | **257,348,947,462.77** | **234,152,498,014.26** | **91%** | **224,394,388,545.88** | **190,147,863,327.02** | **85%** |

| Kiambatisho Namba:4 Matarajio ya Mapato na Matumizi hadi Juni 2026 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATARAJIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ( LIKELY OUTTURN) KWA MWAKA 2025/2026** | | | |
| | **Tarakimu ni TZS "Bilioni"** | | |
| **A: MAPATO** | | | |
| **MAELEZO** | **Bajeti iliyoidhinishwa 2025/2026** | **Matarajio Hadi Juni 2026** | **Asilimia** |
| **Mapato ya Ndani na Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea** | **2,757.235** | **2,687.75** | **97%** |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***2,397.838*** | ***2,327.35*** | **97%** |
| ZRA | 1,257.240 | 1,205.32 | 96% |
| TRA | 825.770 | 825.08 | 99.9% |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 293.829 | 275.95 | 94% |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.000 | 21.00 | 100% |
| ***Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*** | 21.669 | 19.20 | 89% |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)** | 337.727 | 341.20 | 101% |
| ***Mapato ya Washirika wa Maendeleo*** | **1,444.842** | **919.14** | **64%** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 120.000 | 120.00 | 100% |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.539 | 0.50 | 94% |
| Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 361.561 | 225.91 | 62% |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta | 962.742 | 572.72 | 59% |
| **Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** | ***2,780.000*** | ***2,780.00*** | **100%** |
| Mikopo ya Hati Fungani | 1,080.000 | 1,080.00 | 100% |
| Mikopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 1,700.000 | 1,700.00 | 100% |
| **Jumla Kuu** | **6,982.076** | **6,386.88** | **91%** |
| **B: MATUMIZI** | | | |
| **Matumizi ya Kawaida** | ***2,433.267*** | ***2,293.37*** | **94%** |
| Mshahara Mawizara | 810.925 | 804.56 | 99% |
| Mshahara Ruzuku | 142.808 | 142.81 | 100% |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 482.081 | 398.00 | 83% |
| Matumizi Mengeneyo Ruzuku | 108.889 | 79.50 | 73% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 538.337 | 514.90 | 96% |
| Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani | 12.500 | 12.40 | 99% |
| Matumizi ya Taasisi zinazojitegemea | 337.727 | 341.20 | 101% |
| **Matumizi ya Maendeleo** | ***4,539.640*** | ***4,054.41*** | **89%** |
| Fedha za Serikali | 2,919.400 | 2,820.89 | 97% |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | 312.000 | 450.00 | 144% |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 345.498 | 210.80 | **61%** |
| Mkopo Nafuu ya Kisekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 962.742 | 572.72 | **59%** |
| **Jumla Ndogo** | ***6,972.907*** | ***6,347.78*** | **91%** |
| **Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vyao** | ***9.169*** | 6.80 | **74%** |
| **Jumla Kuu** | ***6,982.076*** | ***6,354.58*** | **91%** |
| ***Chanzo Wizara ya*** *Fedha na Mipango* | | | |

| Kiambatisho namba :5 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SURA YA BAJETI 2026/2027 | | | | |
| | TZS Bilioni | | TZS Bilioni | |
| **MAPATO** | **2025/2026** | | **2026/2027** | |
| **Mapato ya Ndani (ikijumuisha na halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **2,757.235** | | **3,611.454** |
| **Mapato ya Kodi na Non Tax** | | **2,397.838** | | **3,249.147** |
| *(i) Mapato ya Kodi -ZRA* | 1,257.240 | | 1,726.661 | |
| *(ii) Mapato ya Kodi - TRA* | 825.770 | | 1,144.690 | |
| *(iii) Mapato yasiyokuwa ya Kodi* | 293.829 | | 356.796 | |
| *(iv) Mapato ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE)* | 21.000 | | 21.000 | |
| **Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa** | 21.669 | 21.669 | 25.996 | 25.996 |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea (Transfer own source)** | 337.727 | 337.727 | 336.311 | 336.311 |
| **Misaada na Mikopo Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** | | **1,444.842** | | **1,514.396** |
| *(i) Misaada ya Kibajeti (GBS)* | 120.000 | | 150.000 | |
| *(ii) Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | 361.561 | | 258.613 | |
| *(iii) Mikopo Nafuu ya Miradi ya Kisekta* | 962.742 | | 1,105.251 | |
| *(iv) Mfuko wa Pamoja (Basket Fund)* | 0.539 | | 0.532 | |
| **Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** | | **2,780.000** | | **3,400.000** |
| *(i) Mikopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo* | 1,700.000 | | 3,400.000 | |
| **Mapato ya Serikali Kuu** | | **6,622.6800** | | **8,163.543** |
| **JUMLA YA MAPATO (A+B+C)** | | **6,982.0761** | | **8,525.850** |
| **MATUMIZI** | | | | |
| **Matumizi Ukijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **2,433.2667** | | **2,737.480** |
| **Matumizi ya Kawaida** | | **2,083.040** | | **2,384.388** |
| **(i) Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali** | **538.337** | | **573.171** | |
| *Malipo ya Riba za Ndani na Mitaji* | 304.640 | | 292.960 | |
| *Matumizi mengineyo ya Mfuko Mkuu wa Serikali* | 233.697 | | 280.211 | |
| **(ii) Mshahara** | **953.733** | | **1,176.327** | |
| *Mshahara Mawizara* | 703.947 | | 920.715 | |
| *Mshahara Ruzuku* | 142.808 | | 139.617 | |
| *Michango ya Serikali katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ( ZSSF)* | 85.582 | | 92.530 | |
| *Mfuko wa Huduma ya Afya ZHSF* | 21.396 | | 23.465 | |
| **(iii) Matumizi mengineyo** | **590.970** | | **634.890** | |
| *Matumizi Mengineyo Mawizara* | 269.801 | | 409.438 | |
| *Matumizi Mengineyo ya Taasisi zinazopokea Ruzuku* | 108.889 | | 119.312 | |
| ***Matumizi maalum kulingana na Sera za Matumizi "Protected Expenditure"*** | 212.280 | | 106.140 | |
| **(iv)Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Mapato ya Ndani** | 12.500 | 12.500 | 16.781 | 16.781 |
| **(v) Matumizi kwa Taasisi zinazojitegemea( Transfer of Expenditures)** | 337.727 | 337.727 | 336.311 | 336.311 |
| **Matumizi ya Maendeleo Ukijumuisha (Halmashauri na Taasisi zinazojitegemea)** | | **4,548.809** | | **5,788.370** |
| **Matumizi ya Miradi ya Maendeleo** | | **4,539.640** | | **5,779.155** |
| (i) Fedha za Serikali Miradi Mipya ya Kimkakati na inayoendelea | 2,427.503 | | 2,863.435 | |
| *(ii) Mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo* | 962.742 | | 1,105.251 | |
| *(iii) Misaada kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo* | 345.498 | | 240.105 | |
| *(iv) Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund)* | 312.000 | | 600.000 | |
| *(v) Miradi Mengineyo* | 491.897 | | 970.363 | |
| *(vi) Matumizi ya Serikali za Mitaa* | 9.169 | 9.169 | 9.215 | 9.215 |
| **Matumizi Serikali Kuu** | | **6,622.680** | | **8,163.543** |
| **JUMLA MATUMIZI (E+F)** | | **6,982.076** | | **8,525.850** |

**Kiambatisho Namba:6**

**MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026-2027/2028**

| | Tarakimu ni TZS "bilioni" | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAELEZO** | **Bajeti Iliyoidhinishwa 2025/2026** | **Makadirio 2026/2027** | **Makadirio 2027/2028** | **Makadirio 2028/2029** |
| **Mapato ya Ndani na Halmashauri** | **2,757.235** | **3,611.454** | **4,354.070** | **5,313.601** |
| **Mapato ya Ndani** | **2,397.838** | **3,249.147** | **3,945.872** | **4,861.697** |
| Mapato ya Kodi - ZRA | 1,257.240 | 1,726.661 | 2,116.294 | 2,637.470 |
| Mapato ya Kodi - TRA | 825.770 | 1,144.690 | 1,391.270 | 1,698.447 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi (Wizara na Taasisi ) | 293.829 | 356.796 | 417.309 | 504.780 |
| Makusanyo ya Kodi za Wanyakazi kutoka SMT (PAYE) | 21.000 | 21.000 | 21.000 | 21.000 |
| ***Mapato ya Halmashauri*** | ***21.669*** | **25.996** | **31.669** | **38.955** |
| **Mapato ya Taasisi zinazojitegemea ( own source)** | ***337.727*** | **336.311** | ***376.529*** | ***412.948*** |
| **Misaada na Mikopo Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** | **1,444.842** | **1,514.396** | **1,124.692** | **1,262.679** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 0.539 | 0.532 | 0.530 | 0.600 |
| Ruzuku kutoka Nje | 361.561 | 258.613 | 354.466 | 319.752 |
| Mkopo kutoka Nje | 962.742 | 1,105.251 | 609.696 | 762.328 |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 120.000 | 150.000 | 160.000 | 180.000 |
| **Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo** | **2,780.000** | **3,400.000** | **3,600.000** | **2,700.000** |
| Mkopo wa Ndani /TB | 1,080.000 | 2,000.000 | 2,000.000 | 1,200.000 |
| Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 1,700.000 | 1,400.000 | 1,600.000 | 1,500.000 |
| ***Jumla Kuu*** | **6,982.076** | **8,525.850** | **9,078.762** | **9,276.280** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **2,433.267** | **2,737.480** | **3,107.998** | **3,575.525** |
| Mshahara Mawizara | 703.947 | 920.715 | 971.381 | 1,100.331 |
| Mshahara Ruzuku | 142.808 | 139.617 | 167.543 | 300.155 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 482.081 | 515.578 | 618.541 | 743.433 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 108.889 | 119.312 | 120.560 | 130.52 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 538.337 | 573.171 | 711.817 | 742.433 |
| Michango ya Serikali katika Mifuko ya Jamii | 85.582 | 92.530 | 99.530 | 99.530 |
| Mfuko wa Huduma ya Afya -ZHSF | 21.396 | 23.465 | 23.638 | 25.870 |
| Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 12.500 | 16.781 | 18.460 | 20.305 |
| Mapato ya Taasisi zinazojitegemea ( own source) | 337.727 | 336.311 | 376.529 | 412.948 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **4,548.809** | **5,788.370** | **5,970.764** | **5,700.755** |
| Fedha za Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | 2,919.400 | 3,833.799 | 4,000.452 | 4200.475 |
| Mfuko wa Kugharamia ulipaji wa Madeni ya Miradi ya Maendeleo | 312.000 | 600.000 | 500.000 | 500.000 |
| Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 1,308.240 | 1,345.356 | 1,457.602 | 981.63 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani | 9.169 | 9.215 | 12.710 | 18.650 |
| **Jumla ya Matumizi** | **6,982.076** | **8,525.850** | **9,078.762** | **9,276.280** |
| ***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango*** | | | | |

**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - 2028/2029**

| SN | TAASISI | Makadirio 2026/2027 | Makadirio 2027/2028 | Makadirio 2028/2029 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Manispaa Mjini | 4,975.89 | 5,533.83 | 6,807.33 |
| 2 | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 3,479.68 | 4,543.23 | 5,766.13 |
| 3 | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 4,275.44 | 5,725.81 | 6,573.15 |
| 4 | Baraza la Manispaa Kaskazini"A" | 3,673.33 | 4,310.30 | 5,710.67 |
| 5 | Baraza la Mji Kaskazini "B" | 1,957.11 | 2,317.34 | 2,743.87 |
| 6 | Baraza la Manispaa Kati | 2,357.29 | 2,575.85 | 2,875.61 |
| 7 | Baraza la Mji Kusini | 2,175.29 | 2,528.71 | 3,144.29 |
| 8 | Baraza la Manispaa Chake Chake | 1,275.48 | 1,765.35 | 2,443.36 |
| 9 | Baraza la Mji Mkoani | 675.09 | 829.01 | 1,018.04 |
| 10 | Baraza la Mji Wete | 525.76 | 782.06 | 944.39 |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya Micheweni | 625.58 | 757.92 | 928.49 |
| | **JUMLA** | **25,995.94** | **31,669.41** | **38,955.31** |

*Chanzo OR-TMSMIM-SMZ*

| MIRADI YA MAENDELEO FEDHA ZA MFUKO WA MIUNDOMBINU KWA MWAKA 2026/2027 ("000") | | |
|---|---|---|
| **FUNGU** | **PROGRAMU/MIRADI** | **MAKISIO** |
| **D01** | **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | |
| | Mradi wa ujenzi wa Masoko ya Kibandamaiti na Kinyasini | 65,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **65,000,000** |
| **L02** | **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | |
| | Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | 24,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **24,500,000** |
| **P01** | **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI** | |
| | **Ujenzi wa Barabara 46.2km zinazoingia katika Maeneo ya Hoteli za Kitalii** | 68,368,734 |
| | **Miradi** | |
| | i) Uwekaji wa Taa kwa Barabara ambazo hazina Taa za Barabarani Mjini na Vijijini | 8,000,000 |
| | ii) Upembuzi Yakinifu wa Uanzishwaji wa Reli Zanzibar na Mpango Mkuu wa Usafiri Tanzania (JICA) | 1,000,000 |
| | iii) Upembuzi Yakinifu wa Ujenzi wa Daraja la Charawe - Chwaka | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **78,368,734** |
| | **JUMLA YA KUBWA** | **167,868,734** |

| Makadirio ya Matumizi kwa Bajeti Inayozingatia Jinsia na Usawa kwa Mwaka 2026/2027 | | |
|---|---|---|
| **S/N** | **Wizara** | **Makisio TZS"000"** |
| 1 | Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi na Utawala Bora | 1,901.738 |
| 2 | Wizara ya Afya | 49,134.217 |
| 3 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 137,977.199 |
| 4 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto | 23,380.743 |
| 5 | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 38,943.385 |
| 6 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo | 5,616.604 |
| 7 | Wizara ya Maji na Nishati | 144,632.054 |
| 8 | Wizara ya Kazi na Uwekezaji | 11.115 |
| 9 | Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji | 48,202.060 |
| | **Jumla** | **449,799.115** |